**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI

**MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA**

**2022/2023**

**MEI, 2022**

**YALIYOMO**

YALIYOMO ....................................................i

ORODHA YA VIAMBATISHO ...............................ii

VIFUPISHO VYA MANENO .................................iv

UTANGULIZI ................................................1

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2021/2022 ........................................6

UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU..................................................7

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2021/2022 ..................................................10

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ...........53

MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023...58

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ..................................................68

HITIMISHO..................................................69

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2021/2022 .........................73

Kiambatisho Nam. 2: Makusanyo ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Taasisi zilizo chini yake .....................................................................76

Kiambatisho Nam. 3: Maeneo yaliyorejeshewa Huduma ya Maji Safi na Salama .......................................77

Kiambatisho Nam. 4: Utowaji wa Elimu kwa watumiaji wa maji........................................................78

Kiambatisho Nam. 5: Utekelezaji wa Mpango wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji kupitia Mfuko wa IMF (Uviko -19)...................................................79

Kiambatisho Nam. 6: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme Unguja na Pemba..............................80

Kiambatisho Nam. 7: Vijiji viliyopelekewa huduma ya umeme Unguja na Pemba ..................................82

Kiambatisho Nam. 8: Hali ya Uingizwaji na Matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa ..............................83

Kiambatisho Nam. 9: Idadi ya Vituo vya Mafuta vilivyopo Nchini ........................................................84

Kiambatisho Nam. 10: Kiwango cha Gesi iliyoingizwa na iliyotumika Nchini (Kg) .......................................85

Kiambatisho Nam. 11: Kiasi cha Tani za Rasilimali zisizorejesheka zilizochimbwa..............................86

Kiambatisho Nam. 12: Mradi wa Uimarishaji Huduma ya Maji Mijini na Vijijini Zanzibar..............................87

Kiambatisho Nam. 13: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 .......................89

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| GWPSA | Global Water Patnership Southern Africa |
| MKUZA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| SDGs | Sustainable Development Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu) |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TZS | Tanzania Shillings (Shilingi ya Tanzania) |
| WMNM | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZANWIP | Zanzibar Water Investment Program |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation (Shirika la Umeme la Zanzibar) |
| ZESTA | Zanzibar Energy Sector Transformation and Access (Mabadiliko ya Sekta ya Nishati Zanzibar na Upatikanaji wa umeme) |
| ZURA | Zanzibar Utility Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar) |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa unyenyekevu mkubwa naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama kwa mara ya kwanza mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

   Kwa mara nyengine tena, namshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutuwezesha kukutana katika kikao hiki adhimu cha kujadili Bajeti tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuzilinda afya zetu sisi na familia zetu.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania. Kwa hakika amekuwa ni mama wa mfano wa kuigwa kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na kuimarisha uhusiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa utendaji

kazi wake uliojaa hekima, busara, juhudi, ubunifu na uadilifu anaoendelea kuuonesha katika uongozi wake. Ni dhahiri kuwa amekuwa chachu ya kuleta maendeleo ya viwanda na uwekezaji hususan katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya kimaendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, vituo vya afya, maskuli, masoko na kadhalika.

4. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu amjalie afya njema yeye na familia yake ili aendelee na moyo wa ujasiri katika kutekeleza misingi ya Utawala Bora katika kufikia azma ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

5. **Mheshimiwa Spika,** aidha, nimpongeze Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna anavyomsaidia vyema Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuongoza na kusimamia shughuli za Serikali katika kipindi chote cha uongozi wake. Kupitia juhudi zake, mageuzi makubwa yameweza kufanyika katika Sekta ya Maji, Nishati na Madini, ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma hizo kwa ufanisi.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kuendelea kuwa Spika wa Baraza la Kumi la Wawakilishi. Ni imani yangu kuwa nafasi hiyo utaendelea kuitumikia ipasavyo na kuitendea haki kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Kadhalika, nimpongeze Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kwa mchango wake mkubwa anaoutoa, ili kuboresha Huduma zinazotolewa na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu. Kadhalika, tunawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza hili kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo. Ni imani yetu kuwa wataendelea kukusaidia katika kuendesha chombo hiki muhimu kwa maendeleo ya wananchi.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Yahya Rashid Mamba, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Khuzaima Mbarak Tahir Mwakilishi wa Viti Maalum Vijana Mkoa wa Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kuchaguliwa kuunda Kamati

hiyo. Kwa hakika, tumekua tukipokea maoni na ushauri mzuri kutoka kwao na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

9. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi kwa Mheshimiwa Abdallah Hussein Kombo kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali. Kadhalika, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kuchaguliwa kuunda Kamati. Tunawashukuru kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri wanaotupatia katika kutekeleza majukumu yetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Shaaban Ali Othman Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Hakika uteuzi wake umeongeza kasi ya usimamizi bora wa huduma za maji, nishati na madini kwa wananchi.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi kuiongoza Wizara hii inayogusa kila mwananchi katika maisha yake ya kila siku.

Naahidi kuwa nitaitumikia nafasi hii kwa nguvu zangu zote katika kuwaletea maendeleo wananchi na kuhakikisha huduma za maji, umeme, mafuta na rasilimali zisizorejesheka zinapatikana na zinaimarika kwa kiwango kikubwa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Manaibu Waziri walioteuliwa na wanaoendelea na nafasi zao katika Wizara mbali mbali. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

12. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika pia, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazolikabili Jimbo letu.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nikishukuru Chama Changu cha Mapinduzi (CCM) kwa namna kinavyosimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 katika kuhakikisha Zanzibar inapiga hatua kubwa za maendeleo. Wizara inaahidi kuendelea kutekeleza programu zake kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021/2026 na miongozo inayoendelea kutolewa na Serikali.

14. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu niwasilishe Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Programu na Shughuli za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2021/2022

***Bajeti na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022***

15. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Idara na Taasisi zilizo chini yake zimetekeleza Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ilivyoidhinishwa katika Baraza lako Tukufu mwezi Juni, 2021 na imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) chini ya Fungu N03. Programu Kuu hizo ni:-

*i.* ***Programu Kuu:*** *Usimamizi wa Huduma za Maji,*
*ii.* ***Programu Kuu****: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini na*
*iii.* ***Programu Kuu:*** *Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM.*

16. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hizi, umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-

2050, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III), Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 (Africa Agenda 2063), Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDG 2030), Ahadi alizozitoa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha Kampeni za Uchaguzi, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na Maagizo ya Utendaji kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu aliyoyatoa wakati wa kuwaapisha na Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayoendelea kutolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

## 2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 98,635,237,000** kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 1,017,500,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 4,845,100,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 92,772,637,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 Wizara imeweza kuingiziwa jumla ya **TZS. 61,649,190,959** sawa na wastani wa asilimia 63 ya fedha zote

kwa kazi za kawaida na Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla ya **TZS. 645,000,000** Sawa na asilimia 63 kwa matumizi mengineyo, **TZS. 3,634,758,259** sawa na asilimia 75 kwa ajili ya mishahara na **TZS. 57,372,432,700** sawa na asilimia 62 kwa miradi ya maendeleo. **Kiambatisho Namba 1 kinafafanua.**

***Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali***

**18. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS. 7,743,262,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na rasilimali zisizorejesheka. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, Wizara imekusanya Jumla ya **TZS. 7,377,085,187** sawa na asilimia 95 ya makusanyo yatokanayo na rasilimali zisizorejesheka. Wizara imeweza kuvuka lengo lilopangiwa katika makusanyo ya miezi tisa. **Kiambatisho Namba 2 kinafafanua.**

**19. Mheshimiwa Spika,** Wizara imevuka lengo la makusanyo yake iliyopangiwa kutokana na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kutoka mfumo wa kupokea malipo ya fedha taslim kwenda mfumo wa kulipia benki.

Vile vile, Wizara imeimarisha usimamizi wa doria za mara kwa mara pamoja na kuwachukulia hatua stahiki wale wote wanaohusika na utoroshaji wa mapato ya Serikali.

***Hali ya Upatikanaji wa Maji nchini***

20. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuboresha sekta ya maji nchini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote wa Zanzibar inaimarika. Kiujumla, hali ya upatikanaji wa maji imeanza kuimarika katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na jitihada za kuimarisha vyanzo vya maji, ili kuongeza uzalishaji wa maji. Hadi sasa, wastani wa uzalishaji wa maji unakadiriwa kufikia asilimia 55 kwa nchi nzima. Kufuatia utekelezaji wa mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (EXIM- INDIA) na mradi wa Maboresho ya Sekta ya Maji kupitia fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya kutekeleza programu ya kuhuisha Ustawi wa Uchumi na Kijamii kutokana na athari zitokanazo na Uviko – 19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), inakadiriwa kuwa kiwango cha uzalishaji wa maji kitaongezeka na kufikia wastani wa asilimia 75 kwa nchi nzima.

22. **Mheshimiwa Spika,** miundombinu yetu ya usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani na maeneo mengine imeendelea kusambaza maji yanayokidhi viwango vya ubora wa maji vya Kitaifa licha ya kuwepo kwa changamoto kwenye baadhi ya maeneo. Changamoto hizo ni pamoja na uwepo wa madini ya chumvichumvi katika maeneo ya Ukanda wa

Pwani. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imefanya Tathmini ya Kubaini Kiwango cha Maji Ardhini (Rapid Assessment on Underground Water in Zanzibar), ili kujua maeneo gani yanaweza kutumika kuvuna maji na kuwapelekea wananchi wanaopata changamoto za maji yenye madini hayo.

23. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara inatarajia kuandaa mpango maalumu kwa ajili ya kuanza hatua za uvunaji wa maji ya mvua kwa lengo la kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Aidha, Wizara inafanya jitihada za kuwekeza katika uimarishaji wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo inayotumia teknolojia za kisasa zenye uwezo wa kupunguza madini ya chumvi ili kufikia viwango vinavyokubalika kwa matumizi ya binadamu.

## 2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2021/2022

24. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini yalikuwa ni pamoja na; kutambua kiwango halisi cha maji kilichopo chini ya ardhi kwa Unguja na Pemba, kuimarisha miundombinu ya maji iliyopo na kuweka

miundombinu mipya, kutambua mahitaji halisi ya maji, kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji wa mapato, kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar na kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa mafuta na gesi Zanzibar.

***MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI***

25. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi kama ifuatavyo:-

***Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji***

26. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

***A. IDARA YA MAENDELEO YA MAJI***

27. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Maendeleo ya Maji ni Idara mpya yenye jukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Maji na kuhakikisha kwamba huduma za maji safi na salama zinapatikana kwa uhakika na endelevu. Aidha, Idara ina jukumu la kufuatilia ubora wa rasilimali maji, usalama wa vyanzo vya maji pamoja na kufanya tafiti za Maendeleo ya Rasilimali za Maji.

Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji imepata mafanikio mbali mbali;

28. **Mheshimiwa Spika,** WMNM imefanikiwa kutembelea maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Kusini na Kaskazini Unguja, ili kutathmini hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo yenye upungufu wa huduma hiyo. Katika ziara hiyo changamoto mbali mbali ziligunduliwa ambazo kwa namna moja au nyengine hupelekea kukwamisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kwa wananchi wa maeneo hayo.

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji imeendelea kushiriki mikutano ya Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa sekta ya maji nchini. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Mkutano wa Wataalamu kuhusu kupitia rasimu ya Sera ya Maji ya Afrika Mashariki na kupitia pendekezo la mradi wa Kikanda kuhusu utekelezaji wa Mkakati Jumuishi wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji (Intergrated Water Resources Management System - IWRMS).

30. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji imefungua milango kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika sekta ya maji Zanzibar. Wizara imefanikiwa kufanya mazungumzo na Kampuni ya AquaPro Tanzania Limited na TPS Energies ambazo zinajishughulisha na ufungaji wa mitambo ya kusafisha maji yanayotoka katika visima vyenye chumvi, bahari, mabwawa na migodi. Katika jitihada hizo, Wizara inatarajia kuandaa muongozo wa utekelezaji wa

Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji, ili kurahisisha wawekezaji kuweka katika miradi ya Maji Zanzibar.

## *B. MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)*

**31. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imefanikiwa kufanya utanuzi na ukarabati wa mtandao wa maji kwa kulaza mabomba kilomita 8.7. Kati ya hizo, kilomita 6 zimelazwa katika maeneo ya Kitogani, Muungoni, Matemwe-Mbuyu Maji, Kariakoo-Michenzani, Kwa Mtumwa Jeni, Sogea na Kilimani kwa upande wa Unguja na kilomita 2.7 zimelazwa katika maeneo ya Kichaka-Nsipwese, Matale, Chokocho na Gombani kwa upande wa Pemba.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kurejesha huduma ya maji safi na salama katika maeneo 36 ya Unguja na Pemba. Kati ya maeneo hayo 12 kwa Unguja na 24 kwa Pemba. Huduma hiyo imerejeshwa katika maeneo hayo baada ya kuweka pampu mpya katika visima vilivyokuwa na hitilafu. **Kiambatisho Namba 3** kinahusika.

**33. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha tatizo la upotevu wa maji linaondoka katika maeneo ya Unguja na Pemba, Wizara imefanikiwa kuziba mivujo 1,681 sawa na asilimia 39 ya mivujo 4,320 iliyopangwa kuzibwa katika maeneo ya Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja mivujo iliyozibwa ni 1,071 na Pemba 610. Aidha, uzibaji

wa mivujo hiyo umepelekea kupunguza upotevu wa maji kwa wastani wa asilimia 3 kwa mabomba yaliyopata hitilafu katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma ya maji safi na salama kwa baadhi ya maeneo kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma hiyo. Jumla ya wateja wapya 5,929 sawa na asilimia 99 ya wateja 6,000 waliopangwa kusajiliwa na kuunganishwa na mtandao wa maji, wamesajiliwa na kuunganishwa na mtandao huo. Kwa upande wa Unguja, wateja waliosajiliwa na kuunganishwa na mtandao wa maji ni 4,302 na upande wa Pemba ni 1,627.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia malipo ya huduma ya maji, ili kuiwezesha sekta ya maji kujiendesha kibiashara. Jambo hili limewekewa msisitizo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Ibara ya 186(b) isemayo "Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usalama wa fedha kwa kufunga mita kwa watumiaji wa maji pamoja na kutumia huduma za kielektroniki katika kulipia huduma hizo".

36. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara kupitia ZAWA imefanikiwa kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari

na mikutano ya Shehia juu ya umuhimu wa kulipia huduma ya maji pamoja na kufahamu changamoto zinazoikabili sekta ya maji. Elimu hiyo imelenga kuwahamasisha wananchi katika kuchangia huduma ya maji pamoja na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoikabili Sekta hiyo. Miongoni mwa Shehia zilizopatiwa elimu kupitia makongamano ni Bububu, Kihinani, Kijichi, Michenzani, Mombasa, Mwanakwerekwe, Kiembe Samaki, Gulioni na Makadara.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2021/2022 jumla ya vipindi vitano (5) vimerushwa hewani kwa njia ya Televisheni na vinne (4) vimerushwa kupitia Redio vinavyohusiana na mada mbali mbali. Aidha matukio ya kihabari pamoja na malalamiko ya wananchi kupitia mfumo wa SNR yameripotiwa na kupatiwa ufumbuzi ikiwa ni katika uimarishaji wa huduma ya maji safi salama kwa wananchi. Uchanganuzi wake umeelezwa katika Kiambatisho Namba 4.

38. **Mheshimiwa Spika,** utoaji huo wa elimu umetoa muamko mkubwa wa kulipia huduma ya maji safi na salama hususan katika maeneo ya mjini. Jitihada hizo zinafanyika kwa lengo la kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa kulipia huduma ya maji safi na salama na uhifadhi wa vyanzo vya maji kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 186 (c na d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025. Naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwenu

Waheshimiwa Wawakilishi kuendelea kushirikiana na Wizara hii na kuunga mkono jitihada za uhamasishaji wa kulipia huduma za maji safi na salama, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za hivi karibuni, Serikali imetenga jumla ya **TZS. 34,200,000,000** kupitia fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya kutekeleza program ya kuhuisha Ustawi wa Uchumi na Kijamii kutokana na athari zitokanazo na Uviko – 19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar. Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya shughuli kuu tatu ambazo ni kuongeza uzalishaji wa maji, ambayo inategemewa kuchimba visima vipya 38, kuviendeleza visima vya RAK 36, kununua na kufunga pampu mpya katika visima 51 kwa lengo la kufikia wastani wa lita **170,696,947** za uzalishaji wa maji ifikapo Juni, 2022. Vile vile, kuboresha na kubadilisha mtandao chakavu wa maji ambapo jumla ya kilomita 319 zinategemewa kufungwa na kubadilishwa. **Kiambatisho Namba 5 kinahusika.**

40. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, kuongeza uhifadhi wa maji kwa kukarabati na kujenga matangi mapya kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya matangi mapya 10 na matangi 3 yatakarabatiwa. Kukamilika kwa matangi hayo kunatarajiwa kuongeza hifadhi ya lita za maji 10,250,000 na kupunguza matumizi ya pampu

kusukuma maji moja kwa moja kwa wananchi (Direct pumping). Wizara inafanya jitihada hizo, ili kuhakikisha kuwa tatizo la uhaba wa maji kwa kiasi kikubwa linapungua na hatimae kuondoka kabisa.

41. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2022 kazi zilizoanza kutekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima kwa upande wa Pemba, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu kwa maeneo 10 ya Unguja na ukamilishaji wa tathmini kwa waathirika wa mradi katika maeneo ya ujenzi wa matangi Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2022 Jumla ya **TZS. 6,373,039,252.60** zimetumika kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi na wasambazaji wa vifaa.

42. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa mifumo ya kupokea na kutatua malalamiko ya wananchi kuhusiana na utoaji wa huduma zake. Mifumo hiyo inahusisha mitandao ya kijamii ya Wizara na ZAWA ikiwemo tovuti ya "Instagram", "Facebook" na "Youtube". Vile vile, Wizara inatumia mfumo wa Sema Na Rais (SNR) katika kutatua changamoto mbali mbali zinazohusiana na utoaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 jumla ya malalamiko 170 yameripotiwa kutoka maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kati ya hayo, malalamiko 80 kupitia SNR yamepatiwa ufumbuzi na yaliyobaki yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

## *MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI*

### *Programu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini*

43. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA). Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi katika sekta hii na kupata mafanikio yafuatayo:-

### *A. SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)*

#### *Hali ya Upatikanaji wa Umeme na Nishati Mbadala nchini*

44. **Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa huduma ya umeme nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2022 jumla ya uniti 356,333,374.43 kWh zimeuzwa kati ya 365,031,556.0 kWh zilizopangwa sawa na asilimia 98 ya mauzo na kupelekea makusanyo ya jumla ya **TZS. 101,156,901,391.16** ambayo pia yamejumuisha na tozo ya VAT.

45. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu nchi yetu inategemea umeme kutoka vyanzo vya umeme vya Tanzania bara, ambapo umeme huo hununuliwa na kusafirishwa kwa njia ya waya

wa chini ya bahari (Submarine Cable) kutoka Ras Kiromoni kuja Fumba kwa Unguja na kupitia Mnyanjani - Majani Mapana Tanga kuja Wesha Pemba. Kwa upande wa Unguja umeme huo hutegemea waya wa chini ya bahari wenye uwezo wa Megawati 100 na Megawati 45 na kwa upande wa Pemba umeme huo hutegemewa kupitia waya wa chini ya bahari wenye uwezo wa Megawati 20.

46. **Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya juu ya umeme yameendelea kukua na kuongezeka kwa wastani wa Megawati tano nukta tano (5.5MW) baina ya mwaka 2012 hadi 2016. Kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, mahitaji yalikuwa yakipanda kwa wastani wa Megawati sita nukta tatu (6.3MW). Mahitaji makubwa zaidi ya umeme yalitokea mwezi wa Julai 2021 na kufikia kiwango cha juu cha matumizi ya umeme (Peak load) cha Megawati (88.4MW). Kutokana na tathmini za Wizara pamoja na ZECO ukuaji huo umeonekana unasababishwa na ongezeko la mahoteli na huduma za kitalii, ukuaji wa sekta za kiuchumi, viwanda na biashara, na kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa umeme nchini.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Zanzibar haiathiriki na kiwango cha juu cha matumizi ya Umeme (Peak Load), ZECO imefanikiwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya Sabmarini Kebo ya zamani yenye uwezo wa 45MW na tayari imeshaanza kupokea wastani wa megawati 25 za umeme kwa sasa. Aidha, ZECO inaendelea

kufanya ukarabati wa transfoma za miundombinu hiyo, ili kuweza kufikia kiwango cha Megawati 35 kitakachotumika kwa waya wa zamani. Juhudi hizo zitaifanya Zanzibar kuwa na sabmarini kebo zenye uwezo wa kusafirisha jumla ya 135MW.

48.**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha kilovolti 33 na kilovolti 11. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 jumla ya urefu wa njia za kusafirisha umeme umefikia kilomita1,383 sawa na ongezeko la asilimia 3.4 ikilinganishwa na kilomita 1,336 zilizokuwa zimefikiwa mwezi Juni, 2021. Kati ya hizo, njia za msongo wa kilovolti 33 ni kilomita 45.1 na kilovolti 11 ni kilomita 2.

49.**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na mambo mengine inajukumu la kusimamia upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wote wa Zanzibar. Katika kufanikisha jukumu hilo, Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) wanaendelea na kazi ya kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi wa Zanzibar.

50.**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2021/2022, Shirika la Umeme limekusanya **TZS. 108,689,057,029.75** sawa na asilimia 84 ya makadirio yaliyowekwa ya **TZS.129,079,892,031**. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya umeme pamoja na

mapato mengineyo ikiwemo gharama za uungaji wa wateja wapya na malipo ya deni la nyuma. Kutokufikiwa kwa lengo hilo, kumetokana na kutokulipwa kwa wakati matumizi ya huduma ya umeme.

51. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kuimarisha Miundombinu ya Umeme, ili wananchi waweze kupata huduma ya uhakika na endelevu. Kwa kipindi cha Julai - Machi, 2021/2022 Shirika lilipanga kutumia **TZS. 12,720,000,000** kwa kazi za uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme. Katika utekelezaji wa kazi hizo, Shirika limetumia **TZS. 11,942,138,006.34** sawa na asilimia 94 kwa kufanya kazi zifuatazo:-

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 Shirika lilipanga kubadilisha jumla ya nguzo mbovu 1,620 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 jumla ya nguzo mbovu 1,859 zimebadilishwa ambazo ni sawa na asilimia 115 ya malengo yaliyowekwa.

    Vile vile, Shirika limefanikiwa kufanya ukaguzi wa Transfoma 853 kwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 71 ya transfoma 1,194 zilizopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Aidha, kupitia ukaguzi huo, Shirika limefanikiwa kurekebisha jumla ya transfoma 48 zilizobainika kuwa na hitilafu (45 kwa Unguja na tatu (3) kwa Pemba).

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Umeme inaendelea kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata umeme wa uhakika na katika kiwango kizuri. Katika kufanya kazi hii, Shirika limeimarisha upatikanaji wa kiwango kizuri cha umeme katika maeneno 43 sawa na asilimia 74 ya maeneo 58 yaliyopangwa kurekebishiwa, ili kupunguza changamoto ya umeme mdogo. Kwa upande wa Unguja maeneo 36 yamerekebishwa na saba (7) kwa Pemba. **Kiambatisho Namba 6 kwa ufafanuzi zaidi.**

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mikakati ya kuhakikisha wananchi wote wanaungiwa umeme na wanafaidika na huduma za umeme nchini. Kupitia azma hio Shirika la Umeme limefanikiwa kuongeza idadi ya wateja wapya na kuwaunganishia huduma ya umeme.

    Jumla ya wateja 21,445 sawa na asilimia 62 ya wateja 34,500 waliokadiriwa kuunganishiwa umeme katika kipindi hicho kwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja wateja 17,525 na wateja 3,920 kwa Pemba wameunganishiwa huduma hiyo.

55. **Mheshimiwa Spika,** idadi ya wateja wapya wanaounganishiwa umeme imeongezeka zaidi kutokana na Serikali kupunguza gharama za kuunganisha umeme pamoja na kufidia gharama za uvutaji wa laini na uwekaji nguzo kutoka kwa wananchi na kubebwa na Shirika lenyewe.

Aidha, ZECO imejenga njia za umeme mkubwa wa msongo wa 33kV zenye urefu wa 41.1km sawa na asilimia 63 kati ya makadirio ya njia iliyopangwa kujengwa (65km). Vile vile, imejenga njia za umeme mdogo wa msongo wa 400kV wenye urefu wa 139.82km sawa na asilimia 95 kati ya makadirio ya njia iliyopangwa kujengwa (148km). Ongezeko hili limetokana na mahitaji ya ujenzi wa njia kuu na idadi kubwa ya wateja wanaovuta umeme.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine ZECO imefanikiwa kusambaza huduma za umeme katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Jumla ya vijiji 36 vimenufaika na huduma hiyo, kati ya hivyo, vijiji 22 Kwa Unguja na vijiji 14 kwa Pemba. **Kiambatisho Namba 7 kwa ufafanuzi zaidi.**

57. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kupunguza upotevu wa umeme kwa asilimia 1.4 kutoka asilimia 17 iliokuwepo mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 15.6 kwa mwaka 2021/2022. Kupungua kwa upotevu huo kumesababishwa na jitihada mbali mbali zilizofanywa na Shirika la Umeme ikiwemo kufanya ukaguzi wa wateja mara kwa mara na kuwafungia mita za mfumo wa kulipa kabla (Pre-Paid).

### B. IDARA YA NISHATI NA MADINI

58. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyoelewa umuhimu wa sekta ya nishati katika maendeleo ya taifa lolote duniani ambapo Zanzibar ni sehemu ya dunia. Kwa kulielewa hilo, sekta hii inahitaji usimamizi imara na uweledi mkubwa ambao utatuhakikishia upatikanaji wa huduma bora za nishati kwa gharama nafuu katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa Zanzibar.

59. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wa Zanzibar unaimarika, Wizara inaendelea na utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Umeme wa Zanzibar (Zanzibar Power Master Plan 2021 - 2050) kwa kutumia wataalamu wake wa ndani. Mpango huu unajumuisha makisio ya matumizi ya umeme pamoja na mpango wa kukidhi mahitaji hayo. Wizara imeshakamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa ambazo zitawezesha kubaini makadirio ya mahitaji halisi ya umeme kwa Unguja na Pemba.

60. **Mheshimiwa Spika,** katika utayarishaji wa Mpango huo, shughuli mbali mbali zimeshafanyika ikwemo tathmini ya maeneo yaliyotengwa kwa uzalishaji wa umeme mbadala, miundombinu ya usafirishaji wa umeme na vyanzo vitakavyowezesha kukidhi mahitaji ya umeme ya Zanzibar kwa siku za baadae. Taratibu za kusawazisha na kuimarisha Rasimu ya Mpango

huo zinaendelea na Rasimu ya awali inatarajiwa kuwasilishwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023.

61. **Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa Mpango huo kutaisaidia Zanzibar kubaini njia bora ya kupata nishati ya umeme wa uhakika na kwa bei nafuu. Kadhalika Mpango huo utatoa muelekeo na muongozo kwa Serikali, Wawekezaji na Washirika wa Maendeleo kuhusiana na aina ya chanzo cha nishati ya umeme kinachohitajika, kiwango cha nishati hio na uzalishaji wa nishati husika. Vile vile, mpango huo utatoa muongozo juu ya usambazaji wa nishati ya umeme kwa wananchi, maeneo ya kuekeza nishati husika pamoja na gharama za uwekezaji katika kila chanzo cha nishati kitakachohitajika kwa Zanzibar.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na nishati ya uhakika na endelevu pamoja na kutekeleza Ibara ya 175 (a) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika Sekta ya Nishati na Nishati Mbadala (Renewable Energy) kutoka kampuni mbali mbali zenye nia ya kuwekeza katika Sekta ya Nishati nchini.

Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 Wizara imefanikiwa kufanya majadiliano kwa njia ya mtandao (video conferencing) na njia ya ana

kwa ana kwa zaidi ya wawekezaji 76 kutoka Nchi mbali mbali. Katika hatua hii, wawekezaji walipata fursa ya kuwasilisha taarifa juu ya uwezo wao wa kuwekeza katika Sekta ya Nishati Zanzibar.

63.**Mheshimiwa Spika,** kupitia majadiliano hayo, Wizara ilibaini kuwa baadhi ya wawekezaji hawakuwa wazi katika utoaji wa taarifa ikiwemo uwezo wao wa kifedha, ufundi, na bei ya kuuza umeme. Hadi sasa, Timu ya kuwasikiliza Wawekezaji ya Wizara imeshafanya tathmini ya wawekezaji na kukamilisha mchujo wa wawekezaji hao.

64.**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo, Wizara iliendelea kufanya majadiliano ya kina na wawekezaji waliofuzu na hatimae kumpata mwekezaji mmoja ambae anatarajiwa kukabidhiwa jukumu la kuendelea na shughuli ya uwekezaji wa nishati ya umeme wa jua katika visiwa vya Zanzibar kwa kiwango cha Megawati 30 katika hatua ya awali. Aidha, Wizara imefanya uchambuzi wa taarifa za mwekezaji huyo pamoja na kuwasilisha taarifa za uchambuzi huo kwa Timu ya Majadiliano ya Serikali (Government Negotiation Team) kwa hatua za ushauri zaidi.

65.**Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango (SMZ) na Wizara ya Fedha na Mipango (SMT) zimefanikisha mazungumzo na Benki ya Dunia (World Bank), ili kuanza utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya

Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Umeme – Zanzibar (Zanzibar Energy Sector Transformation and Access – ZESTA). Aidha, tarehe 14 Disemba, 2021 Benki ya Dunia ilitangaza rasmi kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 142.

66. **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa ZESTA unatarajiwa kujenga njia ya kusafirishia umeme wa kiwango cha kilovolti 132 yenye urefu wa kilomita 100 itakayoanzia kutoka kituo kikuu cha umeme Mtoni hadi Kaskazini na Kusini mwa kisiwa cha Unguja. Sambamba na hilo, Mradi huo utawekeza katika mtambo wa uzalishaji wa umeme wa jua kwa kiwango cha Megawati 18, mtambo wa kuhifadhia umeme (Battery Storage MWh40), kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Sekta ya Nishati pamoja na kupunguza gharama za uunganishaji wa umeme kwa wananchi kutoka **TZS. 200,000** iliyopo sasa na inatarajiwa kushuka zaidi ya kiwango hicho. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka sita tokea kuanza kutekelezwa.

67. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezaji wa mradi huu, mnamo tarehe 17 Februari, 2022 Timu ya utekelezaji wa mradi ikiongozwa na Mratibu wa Miradi ya Sekta ya Nishati kutoka Benki ya Dunia ilifanya kikao na Uongozi wa Wizara kwa ajili ya kufanya majadiliano na kuibua changamoto zinazoikabili Sekta ya Nishati Zanzibar pamoja na kuainisha maeneo yanayohitaji ushirikiano na msaada kutoka Mashirika ya Kimataifa.

Sambamba na hilo, mnamo tarehe 21-25 Februari, 2022 vikao vya Wataalamu wa Benki ya Dunia na Wataalamu kutoka Zanzibar vilifanyika na kujadili maendeleo na muelekeo wa utekelezaji wa shughuli za mradi.

68. **Mheshimiwa Spika,** juhudi hizi zinaenda sambamba na utekelezaji wa Ibara ya 175 (e) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020–2025 ambayo imezungumzia uzalishaji wa umeme wa nishati ya jua kwa kiwango cha Megawati 30 kwa Unguja na Megawati 8 kwa upande wa Pemba.

### *C. MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)*

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar – ZURA ina jukumu la kudhibiti huduma za nishati ikiwemo mafuta na gesi, ili huduma hizo zipatikane kwa kiwango kizuri. Kufuatia jukumu hilo, Wizara imeweza kupiga hatua nzuri katika udhibiti wa nishati pamoja na upatikanaji wa mafuta na gesi kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA, imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 12,215,661,679** sawa na asilimia 71 ya makadirio ya **TZS. 17,200,000,000** yaliyopangwa kukusanywa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022. Makusanyo hayo yanatokana na tozo ya udhibiti wa mafuta na mapato mengineyo

yanayojumuisha (leseni, adhabu na malipo ya uuzaji wa zabuni).

71. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, ZURA ilipanga kutumia jumla ya **TZS. 13,347,357,924.** Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZURA imetumia jumla ya **TZS. 9,432,198,176.48** sawa na asilimia 71 ya makadirio ya matumizi zikiwemo **TZS. 4,500,000,000** ambazo ni mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

    Kiasi hichi cha fedha kilitumika kwa shughuli za kawaida (Recurrent Expenditure). Aidha, kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta, Mamlaka imelazimika kuhaulisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Ofisi - Pemba, ili zitumike katika kupunguza makali ya bei za mafuta.

72. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa huduma za upatikanaji wa mafuta zinaimarika na kuepusha tatizo la uhaba wa mafuta nchini, Wizara kupitia ZURA imebadilisha mfumo wa uingizaji wa mafuta kwa kutumia Makampuni mengi (Multiple importers) na sasa inatumia mfumo wa uingizaji wa mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System – BPS) chini ya Kampuni moja inayoitwa GBP. Mfumo huo umeanza kazi rasmi mwezi Oktoba, 2021. Aidha, usambazaji wa Mafuta kwa jumla unaendelea kufanywa na Kampuni nne (4) za mafuta zikiwemo GAPCO Ltd, Zanzibar Petroleum Ltd (ZPL), United Group

Ltd (UGL) na PUMA Ltd ambazo awali zilikuwa zikiingiza mafuta zenyewe nchini.

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 kiwango cha mafuta kwa jumla kilichoingizwa nchini ni lita 130,073,224 na jumla ya kiwango cha mafuta yaliyouzwa ni lita 134,120,194. **Kiambatisho Namba 8 kinafafanua**. Takwimu zinaonesha kuwa uhitaji wa bidhaa za mafuta nchini unaongezeka ukilinganisha na uwezo wa uhifadhi wa mafuta hayo katika bohari zetu. Aidha, katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, Serikali inatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa kujenga bohari mpya na za kisasa zitazoweza kuhifadhi mafuta kwa wastani wa tani 34,000 katika bandari ya Mangapwani.

74. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha suala la upatikanaji wa mafuta linaimarika nchini, Mamlaka imefanya ukaguzi wa Bohari zote tano (5) kwa Unguja na Pemba (Unguja 4 na Pemba 1) pamoja na kufanya ukaguzi wa vituo vyote 87 vilivyopewa leseni (Unguja 71 na Pemba 16). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 vituo vilivyofungiwa kutokana na kukiuka masharti ni vitano (5) ambavyo ni; Coral Reef (Nungwi), Nungwi Petrol Station, Tunguu Station, Mahonda Petrol Station na Mfenesini Petrol Station. **Kiambatisho Namba 9 kwa ufafanuzi zaidi.**

75. **Mheshimiwa Spika**, ukaguzi huo pia ulihusisha mfumo wa uwekaji alama katika mafuta (Petroleum Marking System) kutoka Bohari za Mtoni na Wesha. Jumla ya mafuta yaliyowekewa alama ni lita 115,381,610 ambazo; Petroli ni lita 72,661,998, Dizeli ni lita 38,511,103 na Mafuta ya Taa ni lita 4,208,509. Aidha, matokeo ya zoezi la uwekaji alama na ukaguzi wa mara kwa mara yamesababisha kupungua kwa uchakachuaji wa mafuta kati ya bidhaa moja ya mafuta na nyengine. Vile vile, kupunguza malalamiko yatokanayo na kuharibika kwa vyombo vya usafiri kutokana na vyombo hivyo kutumia mafuta yaliyochakachuliwa.

76. **Mheshimiwa Spika,** bei ya mafuta katika Soko la Dunia imeendelea kupanda kwa kiasi kikubwa na kupelekea kuathiri soko letu la Mafuta la Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, Serikali kwa kushirikiana na ZURA imepunguza baadhi ya kodi za mafuta na baadhi ya tozo kwa bidhaa ya mafuta kuanzia Septemba, 2021. Aidha, Wizara kupitia ZURA itaendelea kutathmini namna bora ya kupunguza athari za mfumuko wa bei za mafuta katika masoko yetu ya ndani.

77. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imeanza rasmi kudhibiti sekta ndogo ya gesi kwa waingizaji na wasambazaji wa bidhaa ya gesi majumbani. Takwimu zinaonesha kuwa Kampuni tano (5) zinaingiza na kuuza gesi kwa jumla katika visiwa vya Zanzibar ambazo ni; Oryx Gas Tanzania Ltd,

Tp Company Ltd (V-Gas), Lake Gas Ltd, Taifa Gas Tanzania Ltd na Al Nabahan Gas Supply. Kampuni tatu (3) kati ya hizo zina mitambo ya kujazia gesi katika mitungi ambazo ni Oryx Gas Tanzania Limited, TP Company Limited (VGas) na Lake Gas Limited na kampuni zilizobakia hujaza mitungi yake kupitia kampuni zenye mitambo ya kujazia gesi.

Aidha, kampuni tisa (9) zinazosambaza gesi ya kutumia majumbani ni pamoja na Zanzi Gas, Amani Pwani, Furaha General Traders, Gasco Energy, Khaify Trading Company, Samis Gas Network, Sumar Akbar, Al-Nabahan Gas Supply na M - Gas.

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 kiwango cha Gesi ya kutumia majumbani (LPG) kilichoingia nchini ni 4,448,647 Kg, sawa na 4,448 MT sawa na wastani wa 494 MT kwa mwezi na matumizi yake ni 4,288,562Kg sawa na 4,288 MT sawa na wastani wa 476 MT kwa mwezi **Kiambatisho Namba 10 kinafafanua.**

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati, ZURA imeendelea kupokea malalamiko yanayohusiana na huduma za Maji, Umeme, Gesi na Mafuta. Jumla ya malalamiko 45 yamepokelewa na kufanyiwa kazi.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa Sekta na huduma zinazodhibitiwa na ZURA, ZURA imeendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na makongamano ya kijamii kwa kurusha hewani vipindi tisa (9) vya Televisheni na tisa (9) vya Redio ambavyo vinahusu matumizi sahihi na salama ya Gesi ya kupikia (LPG), taratibu za malalamiko kwa huduma zinazodhibitiwa na Usalama katika vituo vya Mafuta.

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Udhibiti wa Huduma za Maji unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imeendelea kudhibiti huduma za maji kwa kufanya ukaguzi wa miundombinu ya maji katika visiwa vya Unguja na Pemba, ili kujua ufanisi wake.

82. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia ukaguzi huo changamoto mbali mbali zimebainika zikiwemo kukosekana kwa uzio na vifaa vya usalama katika vituo vya maji (pump house), uwepo wa makaazi ya watu karibu na vyanzo vya maji, ufungaji ovyo wa wanyama katika maeneo ya vyanzo vya maji na uchakavu wa miundombinu ya maji kwa baadhi ya visima.

Kutokana na changamoto zilizobainika, Wizara imeshachukua hatua za kusawazisha changamoto hizo pamoja na kuomba ridhaa kutoka Serikalini, ili kuyaweka maeneo ya vyanzo vya maji chini ya usimamizi wa Vikosi vya Ulinzi na Idara

maalumu za SMZ kwa lengo la kuyalinda na kuyadhibiti. Usimamizi huo utapelekea vyanzo hivyo visivamiwe na kutumiwa na wananchi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

83. **Mheshimiwa Spika,** ZURA imefanikiwa kuandaa ramani ya utambuzi wa vyanzo na mtandao wa Maji uliopo Zanzibar, ambapo ramani sita (6) zipo katika hatua ya kuchapishwa. Aidha, ZURA imefanya mafunzo kwa wafanyakazi wa ndani kwa lengo la kuwapa uelewa wa kazi zinazofanyika katika Divisheni ya Udhibiti Maji.

84. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, ZURA imefanikiwa kurusha hewani matangazo matano (5) ya Televisheni na matano (5) ya Redio pamoja na Makala mbili (2) za Televisheni, imefanya mikutano tisa (9) na waandishi wa habari kwa ajili ya kutangaza bei ya mafuta pamoja na kutoa taarifa (Posts) 40 katika mitandao ya kijamii na kuimarisha Tovuti. Elimu hizo zimesaidia wananchi kuifahamu ZURA pamoja na kufahamu kazi na maelekezo wanayoyatoa kwao kwa lengo la kuimarisha usalama wa matumizi ya maji na nishati.

85. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukaguzi wa vituo vya umeme, ZURA imefanya ukaguzi wa vituo vinne (4) vya kupozea umeme kutoka Kilovolti 132 kwenda Kilovolti 33 na Kilovolti 11 kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi wa maeneo mbali mbali ikiwemo Mazizini, Jang'ombe, Bambi,

Kilimahewa, Dole na Maruhubi pamoja na maeneo yote ya mjini. Kufuatia ukaguzi huo, Wizara kupitia ZURA imependekeza kuandaa na kuwasilisha kwa wadau miongozo ya mafundi au Kampuni zinazojishughulisha na shughuli za uwekaji wa mifumo ya umeme na kuwataka kutoa maoni yao. Kuendelea na hatua ya kuandaa vigezo vya kiufundi kwa gridi na usambazaji umeme (Grid and Distribution codes).

## D BARAZA LA KUWAWAKILISHA WATUMIAJI WAHUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (COUNSUMER REPRESENTATIVE COUNCIL - CRC)

86. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (CRC) ni miongoni mwa Taasisi zilizoundwa kwa lengo la kutetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

87. **Mheshimiwa Spika,** Baraza hili la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati limeundwa kwa Sheria Namba 7 ya Mwaka 2013 ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ikiwa na jukumu la kutetea na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za maji na nishati, kupokea na kutoa taarifa zinazowahusu watumiaji na kushauriana na watoa huduma, Serikali na Mdhibiti (ZURA) juu ya maslahi ya watumiaji wa huduma za maji na nishati.

**88. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (CRC) limeweza kufanya kazi zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo.

**89. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kutoa elimu kwa jamii juu ya uwepo wa chombo hiki pamoja na haki na wajibu kwa mtumiaji wa huduma za maji na nishati kwa watoa huduma hizo. Elimu hii imetolewa kwa Madiwani na Masheha wa Unguja na Pemba, Taasisi za Kiraia (NGO), Maafisa Habari wa Taasisi za Serikali (PRO) pamoja na waandishi wa habari, wananchi wa vijiji mbalimbali vya Unguja na Pemba, waosha magari na wamiliki wa viwanda vya matofali.

Vile vile, Baraza limefanikiwa kufanya vipindi na kutoa matangazo yanayolenga kulitangaza Baraza katika vituo vya redio na TV mbalimbali zikiwemo ZBC, Redio Kati FM, Assalam FM, Plus FM, Hits FM, Habari FM, Island TV, Redio Jamii Mtegani FM, Zanzibar Cable, Redio Jamii Tumbatu, Redio Jamii Micheweni na Redio Jamii Mkoani.

**90. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kupokea malalamiko na kuyatafutia ufumbuzi. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2021/2022, jumla ya malalamiko 505 yanayohusu huduma za maji na nishati yamepokelewa. Aidha, hatua mbali mbali zimechukuliwa na Baraza katika kutatua malalamiko hayo ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa mlalamikaji (mtumiaji) au

kupelekwa kwa mtoa huduma au kwa mdhibiti wa huduma za maji na nishati (ZURA) kwa hatua zaidi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, jumla ya malalamiko 488 yameshachukuliwa hatua na 17 tu yanayoendelea kutafutiwa ufumbuzi.

91. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limesaidia kutatuliwa changamoto zinazowakabili watumiaji wa huduma za maji na nishati katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Baraza limeshauri ZECO na ZAWA kushughulikia changamoto za umeme mdogo katika maeneo ya Kwarara na Nyarugusu pamoja na tatizo la ukosefu wa maji kwa muda mrefu katika maeneo ya Ndijani na Kikobweni. Aidha, changamoto za maeneo hayo zimeweza kutatuliwa na huduma zimeweza kuimarika katika maeneo hayo.

92. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Baraza linaendelea kulinda haki za mtumiaji, Baraza limetoa ushauri kwa watoa huduma na Mdhibiti juu ya masuala ya huduma za maji na nishati. Miongoni mwa ushauri uliotolewa ni pamoja na kuondowa tozo ya huduma "service charge" na kupunguzwa kwa bei ya kuunga umeme, ili kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi.

Kadhalika Baraza limeendelea kuishauri ZAWA juu ya matumizi ya maji kwa ajili ya kilimo na kutoa ushauri kwa ZURA juu ya kufungwa kwa kituo cha mafuta cha Chasasa Wete Pemba kutokana na mazingira yanayokikabili kituo hicho.

93. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kuimarisha muundo na mfumo wa utendaji kwa kutayarisha nyaraka muhimu za kufanyiakazi kama vile Muundo wa Taasisi (Organization Structure), Mpango Mkakati (Strategic Plan), Mkakati wa Mawasiliano (Communication Strategy), Kanuni za Baraza (CRC Regulations) Sera ya Rasilimali Watu (HR Policy) na Kanuni za Wafanyakazi (Staff Regulations). Nyaraka hizo zitasaidia kufanikisha shughuli za Baraza na kuliendesha kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

94. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kuwa mjumbe katika Umoja wa Mabaraza ya Watumiaji Tanzania (Tanzania Consumer Forum - TCF). Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 Baraza kwa kushirikana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Umoja wa Mabaraza ya watumiaji limefanikiwa kuandaa maadhimisho ya Kitaifa ya wiki ya haki ya mtumiaji duniani inayofanyika kila tarehe 12-15 Machi ya kila mwaka. Maadhimisho hayo yalifanyika Zanzibar ambapo Mgeni rasmi alikuwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Vile vile, Hatua hiyo itasaidia kuimarisha ushirikiano wa kikazi na kisekta juu ya wajibu wa kulinda haki za mtumiaji wa huduma za maji na nishati.

### *MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MADINI*

95. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Madini ni miongoni mwa sekta mpya inayosimamiwa na Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini. Wizara kupitia sekta hii imeweza kusimamia matumizi bora ya rasilimali zisizorejesheka ikiwemo mawe, mchanga, kifusi, kokoto, udongo na vumbi pamoja na kuhakikisha inaondoa uchimbaji holela wa rasilimali hizo. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 Wizara kupitia Sekta hii imepata mafanikio yafuatayo;

96. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kusimamia utaratibu mpya wa upatikanaji wa mchanga ambao unahusisha uchimbaji mchanga katika mashamba ya watu binafsi na kuwawezesha wamiliki wa mashamba yanayotoa huduma hiyo kunufaika moja kwa moja na huduma wanayotoa.

97. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inakuwa na rasilimali ya mchanga ya uhakika na endelevu kwa ajili ya Miradi ya Serikali na Taasisi zake, WMNM imefanya mazungumzo na Wizara ya Madini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kufanikisha upatikanaji wa mchanga maalum (river sand) kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya miradi ya Serikali.

98. **Mheshimiwa Spika,** hadi sasa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanza kuingiza mchanga kutoka Tanzania Bara kuingia Zanzibar kwa ajili

ya kutekeleza miradi mikubwa ya Maji ya ZAWA inayohusisha ujenzi wa matangi makubwa ya kuhifadhia maji pamoja na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya ZAWA. Jumla ya tani 186,000 zimeombwa kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar. Miongini mwa tani hizo, jumla ya tani 80,000 zimeshaingizwa Zanzibar.

99. **Mheshimiwa Spika,** wastani wa tani 5,433,491 za mchanga zimeombwa katika kipindi cha miezi tisa (Julai – Machi, 2021/2022). Kati ya hizo, tani 219,173 zimeombwa kwa ajili ya watu binafsi, tani 1,009,578 zimeombwa kwa ajili ya biashara na viwanda na tani 4,204,740 zimeombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kwa upande mwengine, wastani wa tani za mchanga zilizotolewa kwa kipindi cha Julai – Machi 2021/2022 ni tani 849,609 Kati ya hizo, tani 253,483 zimetolewa kupitia vibali binafsi, tani 102,193 zimetolewa kupitia vibali vya viwanda na tani 493,933 zimetolewa kupitia vibali vya miradi. Takwimu hizo zinaonyesha kwamba, tani za mchanga zinazotolewa ni kidogo ukilinganisha na tani za mchanga zinazoombwa. Tani zilizoombwa na hazikutolewa ni 4,583,882 sawa na asilimia 84 ya tani za mchanga zilizoombwa. **Kiambatisho Namba 11 kwa ufafanuzi zaidi.**

**100. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuandaa warsha ya Wakuu wa Taasisi zinazojihusisha na ujenzi na majengo, ili kuwa na mfumo wa pamoja kuhusiana na mahitaji ya mchanga kwa shughuli za ujenzi. Aidha, Wizara imefanya kikao na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji ya Zanzibar mnamo tarehe 11 Oktoba, 2021 kwa lengo la kujadili suala zima la usimamizi wa rasilimali zisizorejesheka Zanzibar. Kikao hicho, kimeleta tija zaidi ya usimamizi na udhibiti wa pamoja wa rasilimali hizo na kuepusha upotevu wa mapato yatokanayo na rasilimali hizo.

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Sekta ya Madini imeendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kudhibiti biashara haramu ya uchimbaji wa rasilimali zisizorejesheka, ili kuondosha upotevu wa mapato yatokanayo na rasilimali hizo. Kutokana na hali hiyo Wizara imeendelea kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Uchimbaji wa Rasilimali zisizorejesheka kwa kuweka mazingira bora ya utoaji huduma kwa kuzingatia masuala ya usalama katika maeneo ya machimbo.

***Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM***

**102. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Ofisi

Kuu Pemba. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilitekeleza Programu hii kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo;

### *A. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI*

**103. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inakuwa na maono ya muda mrefu, mfupi na wa kati, Wizara inaendelea kuandaa Mpango Mkakati, ili kutoa muongozo wa utekelezaji wa shughuli na programu za Wizara kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mpango huo, umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025, Ahadi za Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021 – 2026).

**104. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu sahihi na zinazoendana na wakati, Wizara inaendelea kukusanya na kuchambua takwimu zenye mnasaba na Sekta ya maji, nishati na madini. Ukusanyaji wa takwimu hizo unasaidia uimarishaji na ustawi wa sekta husika pamoja na kuhakikisha taarifa rasmi kuhusu sekta za Wizara zinapatikana kwa usahihi na kwa wakati kupitia vyanzo sahihi.

**105. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa huduma za maji safi na salama zinaimarika, Wizara imefanya ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa kukagua matangi yote yaliyopo Unguja na Pemba, ili kujua idadi halisi ya matangi pamoja na changamoto zilizopo katika matangi juu ya uhifadhi na usambazaji wa huduma ya maji Zanzibar. Kufuatia ziara iliyofanyika Unguja, imebainika kuna matangi 71. Kati ya hayo, 18 yapo Mkoa wa Kaskazini, 27 yapo Mkoa wa Kusini na 26 yapo Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, kwa upande wa Pemba, imebainika kuna matangi 30. Kati ya hayo, 19 yapo Mkoa wa Kusini na 11 yapo Mkoa wa Kaskazini.

**106. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia ZAWA inaendelea na ukarabati wa matangi yaliyokuwa hayatoi huduma ikiwa ni pamoja na kusawazisha mtandao wa maji unaopeleka maji katika matangi hayo. Vile vile, Wizara inajenga matangi mapya katika maeneo ambayo hayana matangi, ili kupunguza matumizi ya visima kusambaza maji moja kwa moja (direct pumping).

**107. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutembelea maeneo ya mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar kwa lengo la kutathmini hatua za utekelezaji zilizofikiwa katika mradi huo pamoja na kufahamu changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa mradi huo. Kiujumla, utekelezaji wa mradi huo unatekelezwa kwa kasi na unatarajiwa kukamilika ndani ya

muda husika na kuanza kuwanufaisha wananchi wa maeneo ya mradi kama ilivyotakiwa.

**108.Mheshimiwa Spika,** Wizara imeunda Timu Maalumu ya kupitia Sera na Sheria zilizokuwa za muda mrefu na kuzifanyia marekebisho. Miongoni mwa Sera na Sheria hizo ni Sera ya Maji ya mwaka 2004 ambayo tayari imeshafanyiwa mapitio ya awali na taratibu za kumpata Mshauri Elekezi wa kutengeneza Sera mpya zinaendelea. Sera hiyo inatarajiwa kukamilika katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. Vile vile, Wizara imeandaa Rasimu ya Sera ya Nishati ya Zanzibar. Rasimu hiyo imeshajadiliwa katika Vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu na inasubiria miongozo kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa hatua zaidi.

**109.Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Rasimu ya Sheria ya Madini ya Zanzibar. Rasimu hiyo imeshawasilishwa kwa Kamati Tendaji ya Wizara na hatua za kuiboresha zaidi zinaaendelea. Kukamilika kwa Sheria hiyo kutapelekea kuimarika kwa miongozo na taratibu za utoaji wa huduma za Madini pamoja na kuipatia Wizara fursa za kujihusisha moja kwa moja na shughuli za madini hapa Zanzibar.

**110.Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Wizara inakua na matokeo chanya wakati wa utekelezaji wa miradi na program zake imekuwa ikifanya tafiti mbali mbali zenye mnasaba na Sekta za Wizara. Katika kipindi cha Julai – Machi 2021/2022

Wizara imefanikiwa kufanya Utafiti wa Kutathmini Matumizi na Mahitaji ya Maji Zanzibar. Utafiti huu umeweza kukusanya taarifa katika makundi mbali mbali hasa watumiaji wakubwa wa maji safi na salama. Makundi hayo ni pamoja na mahoteli, maeneo ya umwagiliaji, viwanda vya matofali, viwanda vya maji, madrasa na misikiti, bohari za mafuta na maeneo ya kukoshea gari katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

111.**Mheshimiwa Spika,** Kazi ya kukusanya, kuchakata na kuchambua taarifa katika makundi hayo imeshakamilika, hatua inayofuata ni kukamilisha Rasimu ya Awali ya Utafiti huu ambayo inatarajiwa kukamilika Juni mwaka huu.

112.**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa utafiti huu kutaiwezesha Serikali kubaini matumizi na mahitaji halisi ya maji kwa sasa na kwa baadae, ili kuweza kuwafikishia huduma wananchi wote na kujipanga dhidi ya ongezeko la matumizi ya maji linalosababishwa na kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi pamoja na kuhakikisha wananchi wote wa Zanzibar wanapata huduma ya maji safi, salama na ya uhakika.

113.**Mheshimiwa Spika,** sambamba na Utafiti huo, Wizara imefanikiwa kufanya tathmini ya kuangalia kina cha maji kilichopo ardhini "Rapid Assessment on Ground Water in Zanzibar". Tathmini hiyo imefanyika kwa ushirikiano wa karibu na Shirika la Mashirikiano ya Maji Duniani "Global Water Partnership – GWP" pamoja na Wataalamu kutoka

GMI. Tayari Mshauri Elekezi ameshawasilisha Rasimu ya Ripoti ya Utafiti huu na hatua zaidi za kuimarisha ripoti hiyo zinaendelea. Utafiti huo umesaidia sana katika utayarishaji wa Mpango wa Uwekezaji wa Sekta ya Maji Zanzibar (Zanzibar Water Investment Program 2022/2027).

**114.Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mazungumzo na Taasisi ya Ruden AS kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kupata maji safi na salama yatokanayo na visima virefu vya chini ya bahari ambayo yamegundulika kufuatia utafiti wa mafuta na gesi asilia Zanzibar. Wizara imekaa kikao na wataalamu hao tarehe 8 Novemba, 2021 kwa lengo la kupata maelezo kuhusiana na utafiti wa maji chini ya bahari uliofanyika Kimbiji Tanzania.

Vile vile, tarehe 01 Aprili, 2022 Wizara imekaa kikao chengine na Wataalamu hao kwa lengo la kujadili maeneo muhimu ya ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi ya Ruden AS ikiwemo kuboresha miundombinu ya maji itakayoweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi, usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa kijamii pamoja na usimamizi endelevu wa Rasilimali maji. Aidha, Wizara inatarajia kuingia makubaliano (MoU) na Taasisi hiyo, ili kuimarisha uhusiano katika sekta ya maji.

**115. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukuza na kuratibu mashirikiano ya Kisekta na kuhudhuria vikao vya ushirikiano baina ya Sekta za SMZ na SMT. Vikao hivyo vinafanyika kupitia Sekta ya Maji, Sekta ya Nishati na Sekta ya Madini ambapo ushirikiano baina ya Wizara na Sekta husika umeweza kuzaa matunda na kufanikisha mabadilishano ya wataalamu wa maji, ushauri na ujuzi katika kusimamia miradi ya maendeleo pamoja na kujifunza masuala mbali mbali yanayohusiana na Sekta ya Maji, Sekta ya Nishati na Madini kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

**116. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Mashirikiano ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji Duniani (Global Water Partneship - GWP), imefanikiwa kuandaa Kongamano la Viongozi wa Ngazi za Juu la Uwekezaji wa Maji Kusini mwa Bara la Afrika lililofanyika tarehe 11 Machi, 2022 katika hoteli ya Melia Zanzibar.

**117. Mheshimiwa Spika,** Kongamano hilo limeibua fursa za uwekezaji katika Sekta ya Maji na kubainisha changamoto zinazoikabili Sekta hiyo. Kupitia kongamano hilo, Wizara imezindua Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (Zanzibar Water Investment Program 2022-2027). Mpango huo umeainisha na kuelezea mikakati mbali mbali ya uwekezaji katika Sekta ya Maji. Aidha, umeelezea uwekezaji unaohitajika katika kuboresha sekta hiyo na kutoa muongozo kwa miaka mitano ijayo kuhusu maendeleo ya uwekezaji katika Sekta ya Maji.

## *B. IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI*

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na hatua za kuimarisha mazingira ya kazi na wafanyakazi pamoja kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Miongoni mwa stahiki hizo ni mishahara, mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi na kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa Wizara, likizo, mafao ya kustaafu pamoja na malipo ya kujikimu na malazi. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022, jumla ya wafanyakazi 113 wamelipwa mishahara yao, 12 wamekwenda likizo ya kawaida na wamepatiwa posho lao la likizo.

**119. Mheshimiwa Spika,** vile vile, wafanyakazi watano (5) wametengenezewa mafao yao ya kustaafu na kuwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hatua, wafanyakazi watano (5) wamepatiwa gharama za mazishi, wafanyakazi 11 wamepatiwa malipo ya muda wa ziada, wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi wawili (2) wamelipiwa ada ya mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Wizara imefanikiwa kuratibu na kusimamia mafunzo kwa watumishi juu ya Athari za Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na umuhimu wa maadili ya kazi. Kupitia mafunzo hayo, zaidi ya wafanyakazi 80 wamenufaika.

**120. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Idara imefanya tathmini ya kazi kwa watendakazi 60 wa Wizara, ili kujua kwa kiasi gani watumishi wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. Kupitia tathmini hiyo, kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022. Wizara ipo katika hatua za mwisho za utayarishaji wa Mkataba wa Huduma kwa Umma na tayari umeshawasilishwa kwa Kamati ya Uongozi wa Wizara kwa ajili ya kufanyiwa maboresho.

**121. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kuandaa vikao vya Bodi ya Zabuni vya WMNM, Jumla ya vikao tisa (9) vya Bodi ya Zabuni vimeandaliwa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022. Vikao hivyo pamoja na mambo mengine vimejadili Mpango wa Manunuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, mialiko ya Mshauri elekezi (gender specialist) na kuteua wataalamu wa kufanya tathmini ya mshauri elekezi huyo, kupitia hadidu rejea (ToR) ya "Consultancy service for energy efficiency in Zanzibar", kuanzisha mfumo wa madini na kupitia nyaraka za vifaa vya Jiolojia. Mambo mengine yaliyojadiliwa ni kufunguliwa kwa zabuni ya Mtaalamu wa mambo ya Uchumi (Economic Regulation Expert) na zabuni ya mtaalamu wa mambo ya Ufundi (Technical Regulation Expert).

**122. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kuratibu na kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na vikao vya wafanyakazi. Kwa kipindi cha Julai – Machi,

2021/2022, Wizara imeandaa vikao viwili (2) vya Kamati ya Uongozi na vikao vitatu (3) vya Kamati Tendaji na kikao kimoja cha wafanyakazi. Katika vikao hivyo, wajumbe walijadili; Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022; Utekelezaji wa Mpango kazi; Changamoto na fursa zinazopatikana kutokana na Rasilimali zisizorejesheka; kujadili na kupitia Rasimu ya Sheria ya Madini; Uingizwaji wa fedha na mgawanyo wa matumizi na utatuzi wa changamoto za uhaba wa Ofisi za kufanyia kazi.

123. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya Vikao vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu wa Awali na Endelevu katika Ofisi na Idara zote za Wizara. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022, Wizara imefanya vikao viwili (2) vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani ya Wizara. Wajumbe wa vikao walijadili; Mpango wa Ukaguzi wa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani ya Wizara kwa Kipindi cha Januari – Juni 2020/2021.

124. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini ni Wizara ya mpya ambayo haijakamilishwa kuingizwa katika mfumo wa Kanzi Data (Data Base). Maombi ya kuingizwa kwenye Kanzi Data (Database) ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora yamewasilishwa kwa hatua. Sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kuandaa Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano 2022/2027 na kuwasilishwa Utumishi wa Umma kwa hatua stahiki.

## C. AFISI KUU - PEMBA

**125. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba, Afisi Kuu - Pemba imepanga kutekeleza shughuli mbali mbali na kupata mafanikio yafuatayo;

**126. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi kwa wafanyakazi yanaimarika pamoja na kutoa huduma za Uendeshaji na Utawala katika Afisi Kuu - Pemba kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 jumla wafanyakazi 38 wamelipwa stahiki zao. Miongoni mwa stahiki hizo ni mishahara na likizo ambapo wafanyakazi 15 wamepatiwa likizo. Kati ya hao 13 wamepatiwa posho zao kwa wakati na wafanyakazi wawili (2) taratibu za malipo yao zinaendelea. Aidha, wafanyakazi 17 wamefanyiwa tathmini ya utendaji kazi, kwa ajili ya kupandishwa daraja na kuongezewa mishahara.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa upande wa Pemba imeendelea kufanya doria za mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato katika machimbo yaliyopo maeneo ya Pemba. Wizara imekagua maeneo yanayochimbwa mchanga, mawe, fusi, kokoto na matufali ya mawe katika maeneo ya Uondwe, Giningi, Kiungoni, Selemu, Micheweni, Kangagani, Vitongoji, Furaha, Pujini, Mwambe na Uwandani.

Kutokana na uharibifu wa mazingira uliojitokeza kwa baadhi ya maeneo ya machimbo ya Mwambe, Pujini na Furaha. Wizara kupitia Afisi Kuu Pemba imechukuwa hatua ya kuzuiya uchimbaji wa mawe katika maeneo hayo na badala yake kuelekeza uchimbaji huo katika maeneo mengine.

128. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Nishati Mbadala Afisi Kuu - Pemba imefanya ukaguzi wa ujenzi wa hatua ya mwanzo wa "power house" na uzio katika eneo lililojengwa mtambo wa Umeme wa jua katika kisiwa cha Kokota na Njau. Mradi huo umelenga kuzalisha Kilowati 80 na kunufaisha jumla ya kaya 114 kwa Kisiwa cha Kokota na kaya 50 kwa Kisiwa cha Njau. Hadi sasa jumla ya wateja 75 wameshajisajili ambapo 12 wamekamilisha malipo na tayari wameshaungiwa huduma ya umeme katika Kisiwa cha Kokota. Kwa upande wa Kisiwa cha Njau jumla ya wateja 38 wameshajisajili ambapo taratibu za kukamilisha malipo zinaendelea.

129. **Mheshimiwa Spika,** tayari mradi wa kupeleka umeme katika visiwa hivyo umeshakamilika na baadhi ya wananchi wameshaanza kunufaika na huduma hiyo. Kupitia mradi huo, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) limetoa punguzo la gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi wa visiwa hivyo kutoka **TZS. 200,000** hadi kufikia TZS. 50,000, ili kupanua wigo wa shughuli zao za kimaendeleo na kiuchumi.

**130. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Afisi Kuu – Pemba imefanikiwa kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa Shughuli za Afisi Kuu – Pemba pamoja na kufuatilia kwa karibu maagizo yote yanayotolewa na viongozi wakuu wa nchi ikiwemo maagizo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa Ziara zake za Kikazi kisiwani Pemba pamoja na Maagizo ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Aidha, Afisi imefanya ufuatiliaji na tathmini juu ya kazi mbali mbali walizopanga katika Mpangokazi wao kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 pamoja na kufanya ufuatiliaji wa shughuli zilizopangwa na Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa upande wa Pemba.

## 2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**131. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2021/2022 Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimaendeleo na kupata mafanikio yafuatayo;

***i. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar***

**132. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 mradi umeweza kutumia **TZS. 31,733,848,980.48** sawa na asilimia 44 ya makadirio ya **TZS. 72,416,837,000** ya mwaka. Mchanganuo wa matumizi kwa shughuli zilizotekelezwa kupitia mradi huu unaonekana katika **Kiambatisho Namba 12**.

133. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umeanza kutekelezwa mwezi Aprili 2021 na unagharimu USD milioni 92.18 sawa na **TZS. bilioni 211.83** ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Exim ya India. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, Utekelezaji wa mradi huo unaendelea ambapo wakandarasi wamekamilisha uchimbaji wa visima 37 kati ya visima 64 sawa na asilimia 58 ya visima vinavyotarajiwa kuchimbwa katika maeneo ya Masingini (10), Kidutani (13), Dimani (4), Bumbwisudi (4) na Maungani (6). Aidha, ujenzi wa matangi umefikia wastani wa asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika Januari 2023.

Vile vile, kazi za ulazaji wa mabomba kwa mradi mzima imekamilika kwa wastani wa kilomita 94.678. Kazi ya uhakiki na ulipaji wa fidia kwa baadhi ya waathirika wa mradi imefanyika kwa maeneo ya Kwarara- Kongwe, Kwarara-Mpya, Kidutani na Maungani na tathmini kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo mengine ya mradi bado inaendelea.

Aidha Ujenzi wa Jengo la Afisi nao umefikia asilimia 65 ya ujenzi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 tokea kuanza kutekelezwa kwa ujenzi.

### *ii. Mradi wa Kuendeleza Visima vilivyochimbwa kupitia mradi wa Ras El Khaimah*

134. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza visima vilivyochimbwa na Ras El Khaimah. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2021/2022 mradi huu umetumia **TZS. 1,800,189,073.85** sawa na asilimia 23 ya makadirio ya TZS**. 8,000,000,000**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 kazi zilizofanyika kwa upande wa mradi huu ni; Ununuzi wa vifaa vya wellhead (wellhead fittings), ununuzi wa Pampu, Ulazaji wa bomba na Ulipaji wa fidia kwa maeneo ya Upenja, Kibweni, Kandwi, Mkokotoni-Kicheche, Mangapwani, Kangani na Gombani-Mchua umekamilika na kazi ya uhakiki inaendelea kwa Kwale-Gongo.

135. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maji Zanzibar, kwa mwaka ujao wa fedha 2022/2023 Wizara imepanga kutekeleza miradi mengine ya maji na kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma hiyo bila usumbufu. Nawaomba wananchi waendelee kuwa na subra wakati Serikali yao inaendelea na jitihada mbali mbali za kukabiliana na changamoto hizo.

### *iii. Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme Zanzibar (Capacity Building on Maintenance Project) - (CBMP)*

136. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme (CBMP) imefanikiwa kuifanyia matengenezo laini kubwa za umeme zenye mkondo wa kilovolti 33 pamoja na kubadilisha nguzo mbovu ambapo jumla ya nguzo mbovu 1,500 zilibadilishwa ambapo 450 kwa Unguja na 1,050 kwa Pemba. Kadhalika, matengenezo hayo yalifanyika kwa kubadilisha waya chakavu ulio na uwezo mdogo na vifaa vyake vyote kwa kuweka vifaa vipya katika maeneo ya Kivunge hadi Nungwi (17.5km), Kitogani hadi Paje (11.5km) na Dunga hadi Ufufuma (6km) kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba Pandani hadi Masipa (1km), Pujini hadi Kichaka (15km) na Amani road hadi Ole (3km). Matengenezo haya yatasaidia kuondoa kero za wananchi kuhusu kukatika kwa umeme pamoja na umeme mdogo.

### iv. Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Umeme Zanzibar (Zanzibar Energy Sector Transfomation and Acces - ZESTA).

137. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) wameanza utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa

Umeme – Zanzibar (Zanzibar Energy Sector Transformation and Access – ZESTA). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 mradi huu umetekeleza kazi zifuatazo;

i. Kuandaa muongozo wa utekelezaji wa Mradi (Project Implementation Manual – PIM),

ii. Kuandaa jumla ya hadidu rejea 15 kwa ajili ya hatua mbali mbali za utekelezaji,

iii. Kushiriki mafunzo kwa njia ya mtandao ya kutumia mfumo wa manunuzi wa "STEP" wa Benki ya Dunia,

iv. Kuandaa mkataba wa makubaliano baina ya Afisi ya Rais, Fedha na Mipango na Shirika la Umeme Zanzibar na

v. Kuratibu mafunzo ya Uandaaji wa mikataba.

**v. Mradi wa Kuijengea Uwezo Sekta ya Nishati (Zanzibar Energy Sector Support - ZESS)**

**138. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Idara ya Nishati na Madini, ZECO na ZURA chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa gharama za jumla ya "Swedish Kronor 53.6" sawa na TZS. bilioni 14. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2016 ambapo lengo kuu ni kuijengea uwezo sekta ya nishati Zanzibar katika mfumo wa sera, sheria na udhibiti.

**139. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umegawika katika maeneo matano ambayo ni, kuwajengea uwezo Uongozi wa ZECO, kujenga uwezo wa kiuendeshaji na kiufundi kwa ZECO, Kuijengea uwezo Idara ya Nishati na Madini, Kununua vifaa na vitendea kazi vya ZECO pamoja na kuijengea uwezo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) katika masuala ya udhibiti.

**140. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu upo katika hatua za mwisho za utekelezaji ambapo hadi kufikia Machi, 2022 kazi iliyobakia ni ufungaji wa mita 130 zinazoweza kujisoma wenyewe (Automated Meter Reading – AMR) kutoka HEXING ELECTRICAL CO. LTD ya China ambazo zimeshafanyiwa malipo ya awali.

## 3.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**141. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kufanya tafiti za maji zinazohusu mabadiliko na athari za tabianchi;

ii. Kufanya utafiti wa njia mbadala ya kuzalisha maji safi na salama (uvunaji wa maji ya mvua na maji yaliyo chini ya bahari);

iii. Kuanzisha maabara ya kupima ubora wa maji, maabara ya isotopia (isotopes), ili kugundua umri wa maji, kugundua "recharge" na kutambua asili ya uchafuzi wa mazingira (pollution) unaotokea katika vyanzo vya maji;

iv. Kuandaa kanuni na miongozo ya namna ya kudhibiti maji safi na maji machafu pamoja na miongozo wa uunganishaji wa umeme kwenye gridi ya taifa.

v. Kuandaa na kufanya Mapitio ya Sera na Sheria mbali mbali za Wizara.

vi. Kusimamia masuala ya nishati Zanzibar pamoja na Kushiriki katika masuala ya nishati Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na

vii. Kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar.

**142. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo:-

**A. Programu Kuu PN0301: Usimamizi wa Huduma za Maji**

Programu hii itakuwa na Programu Ndogo moja ambayo ni:-

i. Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji.

**143. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, WMNM imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuwezesha uendelezaji, usimamizi na matumizi ya Rasilimali za Maji kulingana na Sera ya Maji na mikakati ya kitaifa,
ii. Kushiriki katika kuandaa, kufuatilia, kutathmini na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo ya maji Zanzibar,
iii. Kutoa miongozo na elimu kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira ya vyanzo vya maji,
iv. Kutoa miongozo kwa wadau kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Maji,
v. Kuibua Miradi ya kimkakati katika kuboresha sekta ya maji na
vi. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua na utafutaji wa vyanzo vipya vya Maji.

**144. Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itatekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo inajukumu la kisheria la kusimamia masuala ya maji hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ZAWA kupitia programu hii imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendeleza kazi za kawaida za matengenezo ya miundombinu ya maji,
ii. Kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji,

iii. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi bora ya huduma ya maji pamoja na umuhimu wa kulipia huduma za maji,

iv. Kusajili wateja wapya na kufunga mita za wateja,

v. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa ZAWA,

vi. Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato,

vii. Kutekeleza Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar (Exim – India 92.18 Million USD ),

viii. Kuendeleza visima vilivyochimbwa na Mradi wa Ras Al Khaimah.

ix. Kutekeleza Mradi wa Maji safi (EXIM-INDIA 35 Million USD) na

x. Kufanya upembuzi yakinifu katika sekta ya maji (KfW 660,000 EUR).

145. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Mamlaka ya Maji Zanzibar imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 10,870,491,200** kutokana na vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya maji na mapato mengineyo.

146. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezwa, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 106,703,257,000** kwa kazi za kawaida na miradi

ya maendeleo. Kati ya hizo **TZS. 408,716,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara, **TZS. 3,608,300,000** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara na **TZS. 102,686,241,000** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo zilizopangwa katika Programu hii.

**B. Programu Kuu PNO302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini**

Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

*i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati.*

*ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.*

**147. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, WMNM imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa huduma za kila siku za uendeshaji na utawala katika Idara ya Nishati na Madini,

ii. Kutoa elimu kwa wananchi wa Zanzibar juu ya maswala ya nishati,

iii. Kuandaa programu za uelewa kwa wananchi na taasisi juu ya matumizi bora ya nishati mbadala na

iv. Kuandaaa Sera na Sheria ya Madini.

**148.Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) na Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (CRC) ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria. Vile vile, Programu hii itatekelezwa na Idara ya Nishati na Madini.

### a) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)

**149.Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuwaunganisha wateja kwenye mfumo wa Geographical Information System (GIS),

ii. Kuwafungia wateja mita za Automatic Meter Reading (AMR), ili kuendana na technolojia mpya,

iii. Kutafuta vyanzo vyengine mbadala vya umeme ili kuondokana na utegemezi,

iv. Kuongeza Uunganishaji wa wateja wapya,

v. Kuendeleza usambazaji wa umeme vijijini,

vi. Kufanya matengenezo ya miundombinu ya kusafirishia na kusambazia umeme na

vii. Kufanya utafiti wa kuweka waya mwengine wa umeme baharini.

**150. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Umeme Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 limejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 182.7 bilioni** kutokana na vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya umeme na mapato mengineyo.

**b) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)**

**151. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ZURA kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuandaa kanuni na miongozo ya namna ya kudhibiti maji safi na maji taka pamoja na muongozo wa uunganishaji wa umeme kwenye gridi ya taifa,

ii. Kutoa mafunzo kwa wadau wa ZURA wanaotumia mifumo inayotengenezwa na Mamlaka,

iii. Kuandaa miongozo ya matumizi bora ya Nishati kwa watumiaji wa kati na wakubwa,

iv. Kufanya tafiti kwa lengo la kuimarisha huduma za sekta zinazodhibitiwa,

v. Kudhibiti kikamilifu huduma za maji na Nishati (mafuta, umeme, na gesi ya kupikia – LPG) na

vi. Kuendelea kukuza uelewa (Raising Awareness) kwa wananchi kuhusu masuala ya udhibiti wa huduma za maji na nishati Zanzibar.

152. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, imejipangia kutumia jumla ya **TZS. 17,384,000,000** kwa kazi za kawaida, Maendeleo na Mchango wa Serikali.

### c) Baraza la Kuwawakilisha Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (CRC)

153. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, CRC kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea na utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kujitangaza na kuwaelewesha watumiaji juu ya haki na wajibu wao, pamoja na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na huduma za maji na nishati.

ii. Kuendelea kufuatilia na kushughulikia malalamiko na kero wanazokutana nazo watumiaji wa huduma za maji na nishati pamoja na kuwasaidia utatuzi wa malalamiko yao kwa watoa huduma.

iii. Kuanzisha Kamati za watumiaji wa huduma za maji na nishati katika kila wilaya za Unguja na Pemba ili kuliwezesha Baraza kuwafikia watumiaji wengi kwa wakati mmoja na kuweza kusaidia kutatua changamoto zao.

## d) Idara ya Nishati na Madini

154. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali zisizorejesheka ambazo ni mchanga, kokoto, mawe, fusi, udongo na vumbi. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara kupitia Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali zisizorejesheka imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. bilioni 10,514,947,000** Makusanyo hayo yanatokana na maombi ya vibali na malipo ya rasilimali hizo.

155. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 26,757,321,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 285,800,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS. 452,741,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 26,018,780,00**0 kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

## C. Programu Kuu PNO303: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM

Programu hii itakuwa na Programu Ndogo Tatu ambazo ni:-

i. *Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM,*

ii. *Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM na*

iii. *Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM – Pemba.*

156. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, WMNM imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi kwa kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao,

ii. Kuandaa na kuratibu mikutano ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya WMNM, vikao vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani na vikao vya Bodi ya Zabuni,

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa WMNM kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi,

iv. Kupokea malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi,

v. Kuratibu na kusimamia mafunzo ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi pamoja na uelewa juu ya athari ya maradhi yasioambukiza kwa wafanyakazi wa WMNM,

vi. Kuimarisha kitengo cha kumbukumbu (Masjala) kwa kukipatia vitendea kazi vya kisasa,

vii. Kuandaa, Kusimamia na Kufanya Mapitio ya Sera, Sheria na Mipango ya kisekta kwa mujibu wa Vipaumbele vya WMNM,

viii. Kuratibu na Kukuza mashirikiano ya Kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za WMNM,

ix. Kufanya Utafiti wa Kubaini Kiwango cha Maji Kilichopo Chini ya Ardhi ya Unguja na Pemba na

x. Kuratibu Utafiti wa Kubaini Matumizi Rasmi ya Umeme kwa Zanzibar.

157. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 1,873,943,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo **TZS. 974,300,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **TZS. 899,643,000** kwa ajili ya Mishahara.

## 3.1 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

158. **Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za WMNM kwa Fungu N03 lenye jumla ya **TZS. 135,334,521,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 1,512,100,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, ***TZS. 5,117,400,000*** kwa ajili ya Mishahara na **TZS. 128,705,021,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Vile vile, naomba idhini ya kukusanya **TZS. 10,514,947,000** kutoka katika

vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na Rasilimali zisizorejesheka. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika **Kiambatisho Namba 13.**

## 4.0 HITIMISHO

**159. Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kwa mara nyengine kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna anavyosimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 kwa vitendo, namna anavyosimamia kwa uadilifu Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa.

Kwa hakika tumeshuhudia mabadiliko makubwa ndani ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miradi ya kimaendeleo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Niwasihi wananchi wenzangu kuendelea kumuunga mkono Rais wetu katika jitihada zake za kutuletea maendeleo, tuwe wavumilivu tukisubiria neema inayoendelea kutekelezwa kupitia Miradi mbali mbali ya Maendeleo nchini. Hii inaonesha wazi nia na malengo ya kuibadilisha nchi yetu katika muelekeo wa Uchumi wa kiushindani wenye kutegemea rasilimali za bahari (Uchumi wa Buluu).

160. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya Hotuba hii akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Dkt. Mngereza Mzee Miraji, Afisa Mdhamini WMNM, Mkurugenzi Mkuu wa ZURA, Mkurugenzi Mkuu ZAWA, Meneja Mkuu ZECO, Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Mkurugenzi Idara ya Nishati na Madini, Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Maji, Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na wafanyakazi wote wa WMNM. Kwa hakika ushirikiano mzuri katika utendaji wao umesaidia kuweza kuiongoza Wizara hii na kutekeleza majukumu yangu kwa uweledi katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanafaidika na huduma za maji safi na salama, Nishati nafuu na ya uhakika pamoja na upatikanaji wa Rasilimali zisizorejesheka kwa shughuli mbali mbali za kijamii na kiuchumi.

161. **Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue nafasi hii kushukuru michango na ushirikiano kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022. Miongoni mwa washirika hao ni pamoja na Benki ya Exim ya INDIA, Benki ya BADEA, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (EU), IMF, pamoja na Taasisi na Mashirika ya JICA (Japan), GWPSA, KfW (Ujerumani), MCC (Marekani), NORAD (Norway), SIDA (Sweden), UNDP, UNICEF, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola na Wadau wengine wa maendeleo.

162. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii. Aidha, napenda pia kuzishukuru Taasisi za Fedha, vyombo vya ulinzi na usalama bila kusahau vyombo vyote vya habari kwa ushirikiano waliotupatia katika kuendeleza Sekta ya Maji, Nishati na Madini.

163. **Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za pekee nizitoe tena kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chake Chake ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunituma tena kuwakilisha maoni na matarajio yao yanayohusu maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Pia, nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na Taifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Niendelee kuwaahidi na kuwahakikishia kuwa nitazidi kuwatumikia kwa kasi zaidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

164. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nichukue fursa hii adhimu kuishukuru kwa dhati familia yangu pamoja na watoto wangu kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

165. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili na kutushauri, hatimae waipitishe Bajeti hii.

166. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara**
**Waziri wa Maji, Nishati na Madini**
**Zanzibar.**

### Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2021/2022

| PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2021/2022 (000) | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2022 (000) | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi wa Huduma za Maji | Idara ya Maendeleo ya Maji | Fedha za Matumizi Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| | | Fedha za Mshahara | | - | - | - | - | - | - |
| | **Jumla** | | | | - | | | - | |
| | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | Ruzuku ya Mshahara | 3,608,200,000 | - | 3,608,200,000 | 2,670,569,084 | - | 2,670,569,084 | 74 |
| | **Jumla** | | **3,608,200,000** | | **3,608,200,000** | **2,670,569,084** | | **2,670,569,084** | **74** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Nishati | Idara ya Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 52,057,000 | - | 52,057,000 | 12,365,000 | - | 12,365,000 | 24 |
| Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Madini | Idara Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 178,343,000 | - | 178,343,000 | 80,317,420 | - | 80,317,420 | 45 |
| | | Fedha za Mshahara | 430,091,000 | - | 430,091,000 | 322,884,345 | - | 322,884,345 | 75 |
| | | | **660,491,000** | | 660,491,000 | 415,566,765 | | **415,566,765** | **63** |
| Utawala na Uwendeshaji wa WMNM | Utumishi na Uendeshaji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 381,800,000 | - | 381,800,000 | 286,313,530 | - | 286,313,530 | 75 |
| | | Fedha za Mshahara | 336,264,000 | - | 336,264,000 | 331,519,895 | - | 331,519,895 | 99 |
| | **Jumla** | | **718,064,000** | - | **718,064,000** | **617,833,425** | - | **617,833,425** | **86** |

| PROGRAMU NDOGO | TAASISI | | BAJETI 2021/2022 (000) | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI,2022 (000) | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti za WMNM | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | Fedha za Matumizi Mengineyo | 215,880,000 | - | 215,880,000 | 168,519,000 | - | 168,519,000 | 78 |
| | | Fedha za Mshahara | 93,951,000 | - | 93,951,000 | 94,546,910 | - | 94,546,910 | 101 |
| | **Jumla** | | **309,831,000** | **-** | **309,831,000** | **263,065,910** | **-** | **263,065,910** | **85** |
| Uratibu wa Utekelezaji wa Shughuli za WMNM-Pemba | Afisi Kuu Pemba | Fedha za Matumizi Mengineyo | 189,520,000 | - | 189,520,000 | 105,000,000 | - | 105,000,000 | 55 |
| | | Fedha za Mshahara | 376,494,000 | | 376,494,000 | 207,723,075 | - | 207,723,075 | 55 |
| | **Jumla** | | **566,014,000** | **-** | **566,014,000** | **312,723,075** | **-** | **312,723,075** | **55** |
| **Jumla Kuu** | | | **5,862,600,000** | **-** | **5,862,600,000** | **4,279,758,259** | **-** | **4,279,758,259** | **73** |

**Miradi ya Maendeleo**

| PROGRAM U NDOGO | TAASISI | BAJETI 2021/2022 (000) | | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2022 (000) | | | % YA FEDHA ZILIZO PATIKANA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | SMZ | WAHISANI | RUZUKU | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi na Huduma za Maji | Mamlaka ya Maji (ZAWA) | 8,652,284,000 | 72,416,837,232 | - | **81,069,121,232** | 1,800,189,074 | 43,908,086,175 | **45,708,275,249** | **56** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa huduma za Nishati | Shirika la Umeme (ZECO) | 5,500,000,000 | 5,745,000,000 | 458,516,000 | **11,703,516,000** | | 11,661,157,451 | **11,661,157,451** | **100** |
| **Jumla ya fedha za miradi** | | **14,152,284,000** | **78,161,837,232** | **458,516,000** | **92,772,637,232** | **1,800,189,074** | **55,569,243,626** | **57,369,432,700** | **62** |
| **JUMLA YA FEDHA KWA WMNM** | | **20,014,884,000** | **78,161,837,232** | **458,516,000** | **98,635,237,232** | **6,079,947,333** | **55,569,243,626** | **61,649,190,959** | **63** |

**Kiambatisho Nam. 2: Makusanyo ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Taasisi zilizo chini yake**

| NA | TAASISI/IDARA | MAKADIRIO YA MAPATO (JULAI - JUNI 2021/2022) | MAPATO HALISI (JULAI - MACHI 2021/2022) | ASILIMIA YA MAPATO HALISI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | IDARA YA NISHATI NA MADINI | 7,743,262,000 | 7,377,085,117.00 | 95 |
| 2 | MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA) | 10,870,491,200 | 2,519,123,782.46 | 23 |
| 3 | SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO) | 170,758,249,727 | 108,689,057,030 | 64 |
| 4 | MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA) | 17,200,000,000 | 12,215,661,679.00 | 71 |
| **JUMLA** | | **206,572,002,927** | **128,281,803,826** | **62** |

**Kiambatisho Nam. 3: Maeneo yaliyorejeshewa Huduma ya Maji Safi na Salama**

| NAM | UNGUJA | NAM | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1 | Bambi – Mpapa | 1 | Wesha |
| 2 | Mwembe Mchomeke | 2 | Gombani |
| 3 | Kilombero | 3 | Machomane |
| 4 | Kitope – Mbaleni | 4 | Bimtumwa |
| 5 | Jambiani | 5 | Mbiji |
| 6 | Donge | 6 | Darajani |
| 7 | Kinduni | 7 | Mtuhaliwa |
| 8 | Bwejuu | 8 | Kwale Gongo |
| 9 | Kianga | 9 | Taifu |
| 10 | Tumbatu | 10 | Shumba Viamboni |
| 11 | U/Ukuu | 11 | Kironjo |
| 12 | Jendele/ Marumbi | 12 | Chanjaani |
| | | 13 | Sharifu Ali |
| | | 14 | Pujini Dodo |
| | | 15 | Ng’ambwa |
| | | 16 | Gando |
| | | 17 | Konde Chemchem |
| | | 18 | Ulenge |
| | | 19 | Ulenge |
| | | 20 | Kengeja |
| | | 21 | Shidi |
| | | 22 | Michenzani |
| | | 23 | Changaweni |
| | | 24 | Kichaka-Sipwese |
| **JUMLA** | | | |

**Kiambatisho Nam. 4: Utowaji wa Elimu kwa watumiaji wa maji**

| Na | Idadi | Mada | Chombo kilichorusha |
|---|---|---|---|
| 1. | Vipindi vitano (5) vya Televisheni | Hali ya upatikanaji wa maji mjini na changamoto zake, Wiki ya maji, Mfumo wa malipo ya maji na hali ya uzalishaji maji. | ZBC na ZCTV, TV Zinjibar. |
| 2. | Vipindi vinne (4) Redio | Mikakati ya uimarishaji wa huduma ya maji, Maadhimisho ya Mapinduzi, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji | Bahari FM, Chuchu FM na Zenji FM |
| 3. | Matukio ya kihabari | Ziara za Mheshimiwa Waziri wa MNM za uhamasishaji pamoja na kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji.<br>Ziara za ukaguzi wa miundombinu ya maji iliyofanywa na Wizara, ZAWA na wageni kutoka Ujerumani, Marekani na Abudhabi.<br>Ziara za kutathmini utekelezaji wa mradi wa India katika maeneo ya Mkorogo, Kidutani, Mfenesini, Maungani, Dimani, Dole na Masingini. | ZBC, TBC, Zanzibar Leo, Hits FM, Bomba FM na Assalamu FM. |
| 4. | Malalamiko kupitia SNR | Jumla ya malalamiko ya 170 yamepokelewa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kati ya hayo 80 yamepatiwa ufumbuzi na yaliobaki yapo katika hatua mbali mbali za utatuzi. | |

**Kiambatisho Nam. 5: Utekelzaji wa Mpango wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji kupitia Mfuko wa IMF (Uviko -19)**

| Na. | Kampuni/Mkandarasi | Kifaa/Kazi | Idadi | Bajet ya Fedha za IMF (TZS.) | Fedha iliyopatiakana | Malipo Yaliyolipwa (TZS.) | Fedha zilizobaki (TZS.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | M/S SAPPHIRE ENGINEERING (T) LIMITED – LOT 3 | 1. GPS RECEIVER | 2 | 573,657,000 | 286,828,500.00 | 286,828,500.00 | - |
| | | 2. ELECTRO FUSION MACHINE | 2 | | | | |
| | | 3. PIPE FUSION MACHINE | 13 | | | | |
| 2 | M/S AMTAS ENTERPRISES – LOT 2 | RIGS | 2 | 1,504,603,044.00 | 752,301,522.00 | 752,301,522.00 | - |
| 3 | M/S SANFRANSISCO GENERAL TRADING ENTERPRIESE – LOT 4 | Pumps | 38 | 1,535,274,881 | 767,667,361.00 | 767,667,361.00 | |
| 4 | M/S SANFRANSISCO GENERAL TRADING ENTERPRIESE – LOT 1 | Pumps | 13 | 622,143,060.00 | 311,610,182.50 | 311,610,182.50 | |
| 5 | M/S GAIA GLOBE ITH. IHR INONU MAH. 0504/3 OF TURKEY – LOT 2 | HDPE PIPE FITTINGS | 150,001 Lupsum | 1,777,793,925.60 | 888,512,158.92 | 888,512,158.92 | - |
| 6 | M/S MUNA NOOR MANUFACTURING AND TRADING LLC – OMAN - LOT 1 | HDPE PIPES | 318,879 mtr | 5,857,116457.50 | 2,927,290,466.17 | 2,927,290,466.17 | - |
| 7 | M/S SHAMJO COMPANY LIMITED | VIBANDA VYA VISIMA – LOT 1 & 2 | 26 | 1,383,395,308.00 | 276,679,061.60 | 276,679,061.60 | - |
| 8 | M/S NIMETA CONSULT (T) LIMITED | MSHAURI ELEKEZI WA UJENZI WA MATANGI – LOT 1,2&3 | 9 Tanks | 890,000,000.00 | 489,500,000 | 162,150,000 | 327,350,000 |

**Kiambatisho Nam. 6**: **Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme Unguja na Pemba**

| NAM. | UNGUJA | NAM. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ubago Jeshini | 1 | Vikunguni Dutani |
| 2 | Tunguu Mahakamani | 2 | Kiongoni |
| 3 | Kianga Skuli | 3 | Wete |
| 4 | Bububu Brilliant | 4 | Fundo Langoni |
| 5 | Shakani Askari jamii | 5 | Pandani Mnarani |
| 6 | Mwera Mji Mwema | 6 | Kiungoni kwa Banyongo |
| 7 | Kianga Chemani | 7 | Hospitali ya Wete |
| 8 | Bububu Kikaangoni | | |
| 9 | Jambiani Mwendawima | | |
| 10 | Taveta banda la mwani | | |
| 11 | Amani Mkoa | | |
| 12 | Kisima Mbaazi | | |
| 13 | K/Samaki Transit | | |
| 14 | Unguja Ukuu Tindini | | |
| 15 | Magirisi kwa Waruguru | | |
| 16 | Mazizini International | | |
| 17 | Jambiani Mfumbwi | | |
| 18 | Mpendae Glorious | | |
| 19 | Fuoni Mambosasa | | |
| 20 | Kinuni Mto Barafu | | |
| 21 | Jumbi Mperani | | |
| 22 | Mbuzini Tumbo Nje | | |
| 23 | Mbuzini Maduka Matano | | |

| NAM. | UNGUJA | NAM. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 24 | Mazizini Kilimo | | |
| 25 | Kisauni Baharini | | |
| 26 | Kisauni Pangani | | |
| 27 | Chukwani Buyu | | |
| 28 | Kianga Sharkia | | |
| 29 | Dole Mnarani | | |
| 30 | Bububu Magengeni | | |
| 31 | Kilimani | | |
| 32 | Fuoni Viwanja vya Walimu | | |
| 33 | Nungwi Baobao | | |
| 34 | Nungwi Skuli | | |
| 35 | Kinumoshi | | |
| 36 | Tunguu Istiqama | | |

**Kiambatisho Nam. 7**: **Vijiji viliyopelekewa huduma ya umeme Unguja na Pemba**

| NAM. | UNGUJA | NAM. | PEMBA |
|---|---|---|---|
| 1 | Moga Kichavyani | 1 | Mleteni |
| 2 | Chanjaani Kigunda | 2 | Mkote |
| 3 | Cheju Zuwiyani | 3 | Mkia Ng'ombe |
| 4 | Bumbwini Midodoni | 4 | Kinazini Mtambwe |
| 5 | Goma | 5 | Likoni Chwale |
| 6 | Kilindi | 6 | Kenya Gando |
| 7 | Muungoni Kisimani | 7 | Chumbuni Msuka |
| 8 | Ubago Uwandani | 8 | Chonja Mji Mpya |
| 9 | Mbaleni | 9 | Kitondooni Kendwa |
| 10 | Ndijani Mseweni | 10 | Pujini Limaanda |
| 11 | Mwache Alale | 11 | Furahia |
| 12 | Bumbwini Kiongwe | 12 | Kimbugu |
| 13 | Bumbwini Pangani | 13 | Mnarani Mantarifu |
| 14 | Unguja Ukuu | | |
| 15 | Fuoni Kibondeni | | |
| 16 | Matemwe Mbuyu Popo | | |
| 17 | Kichwele | | |
| 18 | Jendele Njia ya Cheju | | |
| 19 | Mwera Pongwe | | |
| 20 | Mangapwani | | |
| 21 | Mkwajuni Shindoni | | |
| 22 | Kiboje Uwandani | | |

**Kiambatisho Nam. 8**: **Hali ya Uingizwaji na Matumizi ya Mafuta (Lita) kwa Miezi Tisa**

| MWEZI | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA TAA | JET A-1 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JULAI, 2021 | Yaliyoingizwa | 7,314,252 | 4,257,969 | 437,521 | | **12,009,742** |
| | Matumizi kwa mwezi | 7,907,701 | 4,098,831 | 459,290 | 1,452,000 | **13,917,822** |
| | Wastani wa Mtumizi kwa siku | 255,087 | 132,220 | 14,816 | 46,839 | **448,962** |
| AGOSTI, 2021 | Yaliyoingizwa | 8,508,593 | 4,054,777 | 529,757 | 1,900,703 | **14,993,830** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,134,333 | 4,097,792 | 588,200 | 1,716,000 | **14,536,325** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 262,398 | 132,187 | 18,974 | 55,355 | **468,914** |
| SEPTEMBA, 2021 | Yaliyoingizwa | 9,472,934 | 3,660,937 | 306,946 | 1,907,173 | **15,347,990** |
| | Matumizi kwa mwezi | 7,561,400 | 4,053,222 | 401,500 | 1,144,000 | **13,160,122** |
| | Wastani wa Matumzi | 252,047 | 135,107 | 13,383 | 38,133 | **438,671** |
| OKTOBA, 2021 | Yaliyoingizwa | 5,510,747 | 4,355,935 | 283,973 | | **10,150,655** |
| | Matumizi kwa mwezi | 7,777,380 | 4,109,450 | 412,790 | 1,232,000 | **13,531,620** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 250,883 | 132,563 | 13,316 | 39,742 | **436,504** |
| NOVEMBA, 2021 | Yaliyoingizwa | 9,691,980 | 4,726,103 | 1,067,056 | 1,897,686 | **17,382,825** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,076,600 | 4,377,946 | 538,350 | 1,716,000 | **14,708,896** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 260,535 | 141,224 | 17,366 | 55,355 | **474,481** |
| DISEMBA, 2021 | Yaliyoingizwa | 7,117,524 | 3,869,198 | 525,993 | 1,901,717 | **13,414,432** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,471,500 | 4,303,538 | 487,200 | 2,332,000 | **15,594,238** |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 282,383 | 143,451 | 16,240 | 77,733 | **519,808** |
| JANUARI, 2022 | Yaliyoingizwa | 7,363,986 | 3,794,338 | 380,195 | 3,804,673 | **15,343,192** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,215,069 | 4,178,335 | 394,700 | 2,552,000 | **15,340,104** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 273,836 | 139,278 | 13,156 | 85,066 | **511,336** |
| FEBUARI, 2022 | Yaliyoingizwa | 7,196,396 | 3,403,332 | 1,007,674 | 1,657,299 | **13,264,701** |
| | Matumizi kwa mwezi | 7,804,088 | 4,288,702 | 407,204 | 2,332,000 | **14,831,994** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 278,717 | 153,168 | 14,543 | 83,286 | **529,714** |
| MACHI, 2022 | Yaliyoingizwa | 10,509,856 | 6,006,267 | 0 | 1,649,734 | **18,165,857** |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,495,410 | 4,505,928 | 5,043,228 | 454,507 | **18,499,073** |
| | Wastani wa Matumizi kwa siku | 274,045 | 145,353 | 162,685 | 14,662 | **596,745** |
| **Jumla Ya Mafuta Yalioingizwa Kwa Kila Bidhaa Kwa kipindi cha miezi Tisa** | | **72,686,268** | **38,128,856** | **4,539,125** | **14,718,985** | **130,073,224** |
| **Jumla Ya Mafuta Yaliouzwa Kwa Kila Bidhaa kwa kipindi cha miezi Tisa** | | **72,443,481** | **38,013,744** | **8,732,462** | **14,930,507** | **134,120,194** |

**Kiambatisho Nam. 9**: **Idadi ya Vituo vya Mafuta vilivyopo Nchini**

| | WILAYA | GAPCO | UGL | ZPL | PUMA | SERIKALI | BINAFSI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UNGUJA** | MJINI | 5 | 2 | 3 | | | 3 | 13 |
| | MAGHARIBI "A" | 3 | 3 | 2 | | | 3 | 11 |
| | MAGHARIBI "B" | 1 | 2 | 2 | 1 | | 9 | 15 |
| | KATI | 1 | 3 | 3 | | | 2 | 9 |
| | KUSINI | 0 | 3 | 1 | | | 4 | 8 |
| | KASKAZINI "A" | 2 | 1 | 2 | | | 7 | 12 |
| | KASKAZINI "B" | 1 | 2 | 0 | | | | 3 |
| | **JUMLA NDOGO** | **13** | **16** | **13** | **1** | | **28** | **71** |
| **PEMBA** | MICHEWENI | | | | | | 4 | 4 |
| | WETE | | | | | 1 | 2 | 3 |
| | CHAKECHAKE | | | 1 | | 2 | 3 | 6 |
| | MKOANI | | | | | | 3 | 3 |
| | **JUMLA NDOGO** | **0** | **0** | **1** | **0** | **3** | **12** | **16** |
| **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | | **13** | **16** | **14** | **1** | **3** | **40** | **87** |

**Kiambatisho Nam. 10: Kiwango cha Gesi iliyoingizwa na iliyotumika Nchini (Kg)**

| MWEZI/KAMPUNI | ORXY GAS TANZANIA LIMITED | | LAKE GAS TANZANIA LIMITED | | TAIFA GAS TANZANIA LIMITED | | TP COMPANY LIMITED - V- GAS | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2021/2022** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** | **UINGIZAJI** | **MATUMIZI** |
| JULAI | 408,820 | 404,589 | 34,100 | 40,415 | 0 | 0 | 103,000 | 111,370 |
| AGOSTI | 494,020 | 421,726 | 35,900 | 40,797 | 0 | 0 | 91,620 | 107,882 |
| SEPTEMBA | 443,680 | 436,058 | 40,020 | 37,221 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| OKTOBA | 355,220 | 402,789 | 54,940 | 0 | 16,800 | 0 | 9,263 | 0 |
| NOVEMBA | 388,380 | 358,435 | 34,880 | 0 | 8,880 | 0 | 9,610 | 0 |
| DISEMBA | 376,700 | 418,106 | 36,260 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| JANUARI | 372,380 | 410,143 | 55,320 | 48,182 | 31,650 | 67,365 | 0 | 0 |
| FEBRUARI | 399,780 | 366,955 | 50,294 | 43,194 | 14,400 | 62,030 | 0 | 0 |
| MACHI | 478,560 | 391,696 | 53,320 | 51,749 | 50,850 | 67,860 | 0 | 0 |
| **JUMLA NDOGO** | **3,717,540** | **3,610,497** | **395,034** | **261,558** | **122,580** | **197,255** | **213,493** | **219,252** |

**Kiambatisho Nam. 11**: **Kiasi cha Tani za Rasilimali zisizorejesheka zilizochimbwa**

| MWEZI | MAWE | MCHANGA | KOKOTO | KIFUSI | VUMBI | MATOFALI YA JASI | UDONGO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JUNI | 13,351.0 | 67,375.0 | 6,082.0 | 15,896.0 | 1,962.0 | 969.0 | 0.0 |
| JULAI | 12,369.0 | 64,253.0 | 5,280.0 | 13,852.0 | 1,795.0 | 1,183.0 | 0.0 |
| AGOSTI | 11,138.0 | 56,507.0 | 4,240.0 | 12,370.0 | 894.0 | 1,076.0 | 0.0 |
| SEPTEMBA | 15,068.0 | 63,992.0 | 5,289.0 | 11,408.0 | 1,969.0 | 1,639.0 | 0.0 |
| OKTOBA | 13,888.0 | 74,966.0 | 5,282.0 | 15,065.0 | 1,887.0 | 1,441.0 | 0.0 |
| NOVEMBA | 11,271.0 | 92,751.0 | 4,350.0 | 18,817.0 | 1,761.0 | 1,166.0 | 0.0 |
| DISEMBA | 12,497.0 | 74,525.0 | 5,049.0 | 18,610.0 | 1,747.0 | 936.0 | 0.0 |
| JANUARI | 11,883.0 | 77,406.0 | 4,935.0 | 9,809.0 | 1,662.0 | 862.0 | 113.0 |
| FEBRUARI | 13,802.0 | 88,417.0 | 6,911.0 | 18,098.0 | 2,252.0 | 2,480.0 | 1,913.0 |
| MACHI | 15,631.0 | 117,919.0 | 7,769.0 | 31,813.0 | 4,792.0 | 1,059.0 | 784.0 |
| **JUMLA KUU** | **130,898.0** | **778,111.0** | **55,187.0** | **165,738.0** | **20,721.0** | **12,811.0** | **2,810.0** |

## Kiambatisho Nam. 12: Mradi wa Uimarishaji Huduma ya Maji Mijini na Vijijini Zanzibar

| TAREHE | JINA | MKATABA NO. | ENEO | MAELEZO | CONTRACT AMOUNT | | MAOMBI | | FEDHA ZILIZO PATIKANA | KILICHOLIPWA | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | USD | TZS | USD | TZS | | | |
| | SAFFHIRE ENGINEERING (T) LIMITED | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/02 | LOT 1 | UNUNUZI WA GPS 2 | | 98,648,000 | | 49,324,000 | 49,324,000 | 49,324,000 | - |
| | | | LOT 3 | UNUNUZI WA ELECTROFUSION MACHINE 13 NA GENERATOR 11 (50%) | | 475,009,000 | | 237,504,500 | 237,504,500 | 237,504,500 | - |
| | | | | **JUMLA** | | **573,657,000** | | **286,828,500** | **286,828,500** | **286,828,500** | **-** |
| | AMTAS ENTERPRISES | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/05 | LOT 2 | UNUNUZI WA RIGS 2 ZA KUCHIMBIA VISIMA (50%) | | 1,504,603,044 | | 752,301,522 | 752,301,522 | 752,301,522 | - |
| | | | | **JUMLA** | | **1,504,603,044** | | **752,301,522** | **752,301,522** | **752,301,522** | **-** |
| | SANFRANSISCO GENERAL TRADING | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/02 | LOT 4 | UNUNUZI WA PUMPU ZA KUSUKUMIA MAJI 38 (50%) | **664,909.00** | | 332,454.50 | 767,642,480.51 | 767,969,895 | 767,667,361.41 | 302,533.59 |
| | | | | **JUMLA** | **664,909.00** | | **332,454.50** | **767,642,480.51** | **767,969,895** | **767,667,361.41** | **302,533.59** |
| | M/S GAIA GLOBE ITH. IHR INONU MAH-TURKEY | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 | LOT 2 | UNUNUZI WA HDPE FITTINGS (50%) | **769,607.76** | | **384,803.88** | | 888,896,962.80 | 888,512,158.92 | |
| | | | | **JUMLA** | **769,607.76** | | **384,803.88** | **-** | **888,896,962.80** | **888,512,158.92** | |

| TAREHE | JINA | MKATABA NO. | ENEO | MAELEZO | CONTRACT AMOUNT | | MAOMBI | | FEDHA ZILIZO PATIKANA | KILICHOLIPWA | BAKAA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | USD | TZS | USD | TZS | | | |
| | M/S MOONA NOOR MANUFACTURING AND TRADING LLC - OMAN | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/01 | | UNUNUZI WA HDPE PIPE (50%) | **2,535,548.25** | | **1,267,774.13** | | 2,932,528,305.31 | 2,927,290,466.17 | 5,237,839.14 |
| | | | | **JUMLA** | **2,535,548.25** | **-** | **1,267,774.13** | | **2,932,528,305.31** | **2,927,290,466.17** | |
| 3 | M/S SHAMJO COMPANY LIMITED LOT 1 & 2 - CHAKE CHAKE PEMBA | | LOT 1 | UJENZI WA VIBANDA ( 20%) | | 744,905,166 | | 148,981,033.20 | 148,981,033.20 | 148,981,033.20 | - |
| | | SMZ/IMF/104/W/RNCT/2021/2022/07 | LOT 2 | UJENZI WA VIBANDA ( 20%) | | 638,490,142 | | 127,698,028.40 | 127,698,028.40 | 127,698,028.40 | - |
| | | | | **JUMLA** | | **1,383,395,308** | **-** | **276,679,061.60** | **276,679,061.60** | **276,679,061.60** | **-** |
| | | | | | | | **1,985,032.51** | **1,315,809,085.41** | **5,905,204,246.71** | **5,899,279,070.10** | |
| | SANFRANSISCO GENERAL TRADING ENTERPRISES-DUBAI, UAE | SMZ/IMF/104/G/RNCT/2021/2022/02 | LOT 1 | UNUNUZI WA PUMPU ZA KUSUKUMIA MAJI 13 (50%) | **269,326.00** | | **134,663.00** | | 311,610,182 | 311,610,182.50 | - 0.50 |
| | | | | **JUMLA** | **269,326.00** | **-** | **134,663.00** | **-** | **311,610,182.** | **311,610,182.50** | **- 0.50** |
| | M/SNIMETA CONSULT (T0 | SMZ/IMF/No.104/CS/RNCT/2021/2022/08 | | MSHAURI ELEKEZI UJENZI WA MATANGI (55%) | | 890,000,000 | | 489,500,000 | 489,500,000 | 162,150,000.00 | 327,350,000.00 |

**Kiambatisho Nam. 13**: **Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| | MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | RUZUKU YA MSHAHARA | UENDESHAJI WA OFISI (OC) | MAKISIO YA SMZ | MHISANI | RUZUKU | JUMLA |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | **156,716,000** | **3,608,300,000** | **252,000,000** | **85,010,541,000** | **17,675,700,000** | **-** | **106,703,257,000** |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji | 156,716,000 | 3,608,300,000 | 252,000,000 | 85,010,541,000 | 17,675,700,000 | - | 106,703,257,000 |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **452,741,000** | **-** | **285,800,000** | **14,729,000,000** | **11,289,780,000** | **-** | **26,757,321,000** |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Nishati | 452,741,000 | - | 237,235,000 | 14,729,000,000 | 11,289,780,000 | - | 26,708,756,000 |
| Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Madini | | | 48,565,000 | | | | 48,565,000 |
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WMNM** | **899,643,000** | **-** | **974,300,000** | | | | **1,873,943,000** |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 411,066,000 | - | 420,800,000 | - | - | - | 831,866,000 |
| Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za WMNM | 91,581,000 | - | 253,500,000 | - | - | - | 345,081,000 |
| Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM-Pemba | 396,996,000 | - | 300,000,000 | - | - | - | 696,996,000 |
| **JUMLA KUU** | **1,509,100,000** | **3,608,300,000** | **1,512,100,000** | **99,739,541,000** | **28,965,480,000** | **-** | **135,334,521,000** |

## Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 – 2022/23

| IDARA YA NISHATI NA MADINI - UNGUJA | | |
|---|---|---|
| **AINA YA MAKUSANYO** | **MAKISIO (2022 - 2023)** | **MAKISIO (2022 - 2023)** |
| Vibali | 127,650,000 | 154,687,000 |
| Ada ya Mchanga, Mawe na Kokoto | 6,772,312,000 | 9,009,668,000 |
| Nyaraka za Zabuni | - | 500,000 |
| Faini | - | 50,100,000 |
| **JUMLA** | **6,899,962,000** | **9,214,955,000** |
| **AFISI KUU - PEMBA** | | |
| | **MAKISIO (2021 - 2022)** | **MAKISIO (2022 - 2023)** |
| Vibali | 15,601,000 | 26,000,000 |
| Ada ya Mchanga, Mawe na Kokoto | 827,699,000 | 1,248,992,000 |
| Faini | - | 25,000,000 |
| **JUMLA** | **843,300,000** | **1,299,992,000** |
| **JUMLA YA MAKUSANYO YA WIZARA** | **7,743,262,000** | **10,514,947,000** |